

MUNGU ANAYO NJIA

ILIYOANDALIWA



Habari za asubuhi, marafiki. Tuna furaha kuwa hapa asubuhi ya leo, maskanini, tena, katika Jina la Bwana Yesu, kuwahudumia watu Wake, kwa Neno lililoandikwa na kwa maombi kwa ajili ya wagonjwa. Nimechelewa kidogo tu, mimi mwenyewe, ku—kuonekana.

² Na nina furaha sana kuwa hapa na kuona siku hii nzuri, ninyi nyote mmetoka mkamtumikie Bwana. Mimi... Je, hamna furaha kwamba mna nguvu za kutosha kuwa kanisani, asubuhi ya leo? Mnaona, kuna watu wengi ambao hawangeweza kuja. Wanafungulia simu kule nyumbani, mchana kutwa, na kuwasikiliza tu watu. Wanawaambia, aisee, “Vema, Jumapili asubuhi tunawaomba wagonjwa kule maskanini.” Watu wanaoingia, mbona, hawajatembea kwa miaka mingi. Wazia tu, halafu, wewe unaweza kuwa hapa leo. Ni jambo la heri jinsi gani kuweza kutoka nje!

³ Mnajua, kulikuwa na msemu wa zamani niliosoma wakati mmoja, ulisema, “Nililalamika juu ya kutokuwa na viatu hata nilipomwona mtu ambaye hakuwa na miguu.” Kwa hiyo, ndivyo hivyo. Kama ukiangalia pande zote, daima kuna mtu ambaye ana hali mbaya zaidi kuliko yako. Basi hiyo ni...

⁴ Lakini kuwazia, asubuhi ya leo, juu ya mambo yote kwamba tuna Mwokozi mwenye upendo, ambaye anatupenda na anatushughulikia, na kujua ya kwamba kazi hii kubwa sana tunayopitia, na nyakati na matatizo tuliyo nayo, ni negativu tu ya safari hii. Na kwamba siku moja tutapokea mwili ambao hautaugua kamwe, wala hautazeeka. Hautawahi kuwa... Na kamwe hatutatengana. Daima tutakuwa pamoja.

⁵ Ninapenda ushirika. Kila mtu, naamini, hasa Wakristo, wanapenda ushirika. Na kuwazia juu ya ushirika wetu wa ajabu! Na, halafu, siku moja tutakuwa pamoja, kamwe haitatulazimu kuondoka, kamwe haitatubidi kuondoka. Kamwe hatutakuwa na wasiwasi kama watoto wataumia au chochote kile, itakuwa... Hakutakuwa na kitu kama hicho. Itakuwa tu... Kamwe hatutasumbuka vyakula vyetu vinatoka wapi; daima vimeandaliwa na kuwekwa tayari kwa ajili yetu. Na hiyo si ni ajabu sana? Katika wakati huo mkuu utakaokuja. Na hiyo ndiyo sababu tuna makanisa, na—na Roho Mtakatifu yuko hapa leo, a—akiwavuta watu kwenye moyo wa Mungu, kuwatayarisha kwa ajili ya wakati huo. Ni wale wanaofanya uamuzi wao sasa, kwa upande huo, ndio watakaofurahia baraka hizo Milele.

6 Nami ninaamini kwamba kama kuna mtu yeyote hapa, leo, ambaye hajawahi kufanya uamuzi wa namna hiyo kumtumikia Bwana Yesu, kwamba hii itakuwa siku ambayo utaufanya. Na, tangu leo na kuendelea, utajiunga na kundi hili kubwa la waaminio, na kusonga mbele kuelekea kwenye ushindi. Siku moja itakwisha.

7 Ndugu Fleeman, ninaamini kuna be—be—benchi papa hapa, ikiwa ungependa kuichukua hiyo sasa, labda ungeweza kuikalia. Hiki hapa kiti kimoja. Sisi. . . Maskani yetu ni ndogo sana hapa, hatuna nafasi ya kutosha kwa watu. Lakini, bado, kuanzia Ijumaa usiku na kuendelea, kwa kawaida tunajaribu kuwaleta, na kuwaleta mahali tunapoweza kuwaombea humu maskanini Ju—Jumapili asubuhi.

8 Nao ulimwengu, bila shaka tuna ulimwengu mgonjwa, watu wengi, magonjwa, matatizo, dhiki. Lakini, kama tusemavyo, kuna wakati mmoja ambapo hayatakuwako tena. Je, si litakuwa jambo zuri sana wakati kamwe hatutawaombea wagonjwa tena, kamwe hatutamwombea mwenye dhambi? Yote yamekwisha, yote yametoweka, katika mambo makuu yaliyosahaulika ya wakati huo, na ndipo tutaishi pamoja Naye.

9 Sasa, tunajua ya kwamba kuna msongamano kidogo hapa ndani. Na la—laiti tungeliwafanya mstarehe zaidi, lakini hatuwezi. Kwa hiyo tunaomba tu kwamba Baba yetu wa mbinguni mwenye fadhili, atakuchangamsha sana moyoni mwako, kwa Uwepo Wake, hata hutaona hii hali ya kubanana ambayo inakubidi kuketi wakati ibada zinapoendelea. Na ustarehe sana ndani Yake!

10 Na sasa, leo, tutajifunza kutoka kwenye Neno kwa dakika chache, ndipo tuwaombe wagonjwa na wahitaji. Hasa, huduma yangu. . . Mimi sana sana si—si mwalimu, kutoka kwa Neno la Mungu, na labda sijui mengi sana kuhusu Kitabu Chake. Lakini, kama ninavyosema mara nyingi, namjua Mwandishi wake vizuri sana. Na hilo ndilo jambo kuu. Na—nataka kumjua Yeye.

11 Kumjua Yeye ni Uzima. Na mimi—mimi ninao Uzima kwa kumjua; Uzima wa Milele udumuo, usioweza kuangamia. Ni wa milele. Mungu hutoa karama Yake ya Uzima wa Milele, na ni mwema milele. Hauharibiki kamwe, na kamwe hautazeeka na kufifia. Mwili wako utazeeka siku moja, ikiwa utaishi. Lakini nafsi yako, roho yako, haitazeeka kamwe.

12 Nilikutana na mzee mmoja wakati mmoja, ambaye alikuwa amepita miaka mia moja kwa mbali, na akasema amekuwa Mkristo tangu alipokuwa na umri wa miaka saba. Nami nikasema, “Ndugu, vipi, uko namna gani leo?”

13 “Loo,” akasema, “Ndugu Branham, Yeye anazidi kuwa mtamu kadiri miaka inavyosonga.” Karibu umri wa miaka mia moja na minne, au mitano.

¹⁴ Ndipo nikawazia, “Bado ni mtamu kadri miaka inavyosonga,’ yapata miaka tisini na saba, tisini na nane, ya kumtumikia Bwana, na Yeye bado alikuwa mtamu zaidi.” Nawazia, nyakati zinapoendelea mbele, Yeye bado atakuwa bora kila wakati; tunapotazama nyuma na kuona yale Mungu ametupitishia, na kututoa kwake, na kutuingiza ndani.

¹⁵ Maisha ya Ukristo ni sa—safari. Hii ni safari hapa, nasi tunapitia tu katika nchi hii. Nasi ha—hatutakaa hapa, mnajua hilo. Mara nyingi tunajenga nyumba, tunasema, “Naam, mimi na familia tutatulua hapa chini.” Lakini, vipi, kwa muda gani? Mnaona? Hujui. Nasi sikuzote tungependa kupata mahali ambapo tunaweza kusema tu, “Hapa ni petu, daima.” Lakini sio hapa, duniani. Hatuna mahali pa namna hiyo hapa duniani.

¹⁶ Lakini kuna kitu ndani yako kinachoitia mahali hapo. Na kabla hapajawa na kitu chochote ndani yako kinachoitia mahali hapo, mahali hapo hapana budi pawepo, la sivyo kusingekuwako na kitu hapa ndani kinachopaita. Kilindi hakiwezi kuitia Kilindi isipokuwa kuna Kilindi cha kuitikia. Kwa hivyo lazima kuwe na kitu ndani, kinachoitia mahali fulani, kabla . . . Hapana budi pawe na Mahali kwanza, hasa, kufanya kilindi hiki kipaite, halafu wakati kuna kitu hapa ndani kilicho na shauku.

¹⁷ Sasa ninaona baadhi ya marafiki zangu ambao nimekua pamoja nao, pia, tumekulia pamoja hapa. Nami nawazia, miaka michache iliyopita, wavulana wadogo wakicheza gololi huku nje mitaani, na kuzungusha pia, kupanda farasi, na leo hii tumeufikia umri wa makamo. Halafu ninaona baba zao, wawili ama watatu, wameketi hapa asubuhi ya leo, hiyo ni, loo, walipokuwa vijana, wanaume wenye nywele nyeusi, na leo hii wameketi hapa wakitetemeka na ni wakongwe. Na hatuna budi kukabiliana na tukio hilo la kutetemeka na la kizee. Lakini mmoja baada ya mwingine, tunazunguka-zunguka chini, ni wasafiri tu na wageni, tunapita. Sasa, jambo la heri hapa ndani, ambalo . . .

¹⁸ Nilikuwa nikizungumza na msichana fulani muda mfupi tu uliopita, ambaye alikuwa anaugua ugonjwa wa fadhaa, na huo ugonjwa wa fadhaa. Mimi . . . Alisema jinsi alivyojaribu kuushinda. Sasa, mimi si Mwanasayansi wa Kikristo au wa Umoja. Si—siamini kwamba kuna kitu kama akili kuushinda mwili. Ninaamini Mungu ndiye mponyaji. Sasa, mimi . . . Msichana huyo alizaliwa katika hali hiyo ya fadhaa. Mama yake na baba yake walikufa alipokuwa mtoto, mtoto mchanga, na akalelewa, akirushwa-rushwa tu kila mahali, wala hakuwahi kupata upendo na malezi mazuri anayopata mtoto.

¹⁹ Unajua, mama, nataka kukwambia jambo fulani. Ninajua nina mvulana mdogo huko nyuma, na ameharibika sana, lakini afadhali niwe naye hivyo. Ninaamini itamfanya mtu bora zaidi,

Mungu akimjalilia kuishi, kuliko kumwacha apige makelele na kulia, na kuudhi utu wake mdogo.

²⁰ Sikilizeni, miaka michache iliyopita, baadhi ya waganga wa kisasa wa jadi walisema, ya kwamba, “Acha mtoto huyo mchanga alie. Usimbebe. Katika mambo haya yote—yote namna hiyo, usimruhusu nyanya amguse.” Nanyi mwajua walichoangua? Mnaona ni nini? Uhalifu wa vijana, kundi la wendawazimu.

²¹ Mungu alimfanya mtoto mchanga apendwe. Ndiyo maana alimfanya mama ampende mtoto mchanga. Ndiyo maana tu—tunapaswa kuwa hivi. Mungu alilifanya hivyo. Na wakati wowote unapovuruga mpango wa Mungu, inakubidi ukumbuke umekosea na utakuwa makosani, maadamu unavuruga mpango wa Mungu. Fuata mpango wa Mungu. Ufanye jinsi Mungu alivyosema ufanywe. Sasa, njia pekee ambayo hilo linaweza kuwa...

²² Kama vile tu, wewe ulizaliwa mwenye dhambi. Na njia pekee ambayo unaweza kuwa chochote kingine ila mwenye dhambi, haina budi kuwa ni kuzaliwa kwingine. Huna budi kuzaliwa Mkristo. Kama ulizaliwa mwenye dhambi, basi huna budi kuzaliwa uwe Mkristo. Na haina budi kuwa ni kitu kinachotendeka ndani yako.

²³ Na hilo ndilo jambo lile lile ambalo halina budi kutukia katika uponyaji wa Kiungu. Ni lazima iwe ni kitu fulani kinachotendeka, si kuchochewa tu au mhemuko. Haina budi kuwa ni kitu fulani ambacho kinatokea, na unajua kinatokea. Unaona? Sio tu, “Loo, vema, nitaliwazia tu *hivi*, na kulisoma *hivyo*.” Hiyo haifai kitu. Haina budi kuwa ni kitu kinachotokea kweli.

²⁴ Sasa, leo hii, na tunatarajia magari ya kuchukulia wagonjwa kadhaa yaliyojaa watu kuingizwa ndani, katika dakika chache, wanaokuja kwa ndege. Nasi tunataka kuingia katika somo moja asubuhi ya leo, kwa wale walioko hapa, ambao ni wagonjwa sana na wahitaji, juu ya somo la uponyaji wa Kiungu, ili imani yako iweze kujengwa juu ya uponyaji wa Kiungu, kujua ni nini hasa, na kujua la kufanya, jinsi ya kufanya mipango ili—ili kujiandaa kwa ajili ya uponyaji wako.

²⁵ Ni wangapi waliosoma *Maisha Ya Kikristo*, mwezi huu? Je, mlipata kulisoma, lile jarida la *Maisha Ya Kikristo*? Ninaamini...La, samahani. Nililipata mwezi huu, lakini lilitumwa kwangu. Juu ya daktari maarufu huko Illinois, aliyeulizwa swali, “Vipi kuhusu uponyaji wa Kiungu?” Laiti ningalikuja nalo, asubuhi ya leo. Naye akasema, “Je, kuna kitu kama hicho?” Wakamwuliza, “Je, kuna kitu kama uponyaji wa Kiungu?”

26 Akasema, “Bila shaka.” Na ikiwa daktari huyo hakuelezea jinsi hasa nilivyolielezea! Kuhusu mkono wangu kukatwa, kwamba haijengi tishu; dawa.

27 Tu—tunafikiri dawa ni nzuri sana. Wala tusingesema, “Usiitumie.” Kwa sababu, ni kitu...Kama tu, nisingesema, “Usitumie sabuni kuosha mikono yako.” Ni kemikali. Lakini, hata hivyo, dawa haiponyi. Dawa husafisha tu, huku Mungu akiponya.

28 Huwezi kufunga mkono wako, wala Daktari hawezi kuingia na kufunga mkono wako, aseme, “Sasa umepona.” Anaufunga tu mkono wako, kisha anaenda zake na kumwacha Mungu akuponye. Hivyo tu ndivyo inavyoweza kufanywa.

29 Naam, sasa, hivyo ndivyo ilivyo kwa kunywa dawa. Lakini, dawa ni sawa, ni sawa kufunga mkono wako kama ukiuvunja, lakini Mungu hana budi kufanya uponyaji. Naam, sasa, hii ni...

30 Uponyaji huu, huna budi kuwa na imani. Unaitwa uponyaji wa imani. Basi daktari huyu alisema, “Vema, kuna kitu kama miujiza.” Akasema, “Nami nimeiona, mara nyingi.” Alikuwa daktari maarufu wa upasuaji. Akasema, “Mara nyingi...” Akasema, “Sasa, unapokuja kwenye madhehebu yasiyo na Damu, wanaosema kwamba mtu fulani anafanya hivyo, au—au kitu kama wa Umoja, na kadhalika,” kasema, “Nisingegusa hilo hata. Lakini,” kasema, “ninaamini, na ninajua, ya kwamba Damu ya Yesu Kristo inatosha kabisa kuponya ugonjwa wowote.” Mnaona? Sasa, inakuja kwa njia ya Kristo. Uponyaji unatoka kwa Kristo, peke yake. Na wote unakuja...Ikiwa wongofu wako...

31 Sasa, nimeona watu waliojifanya, wakasema, “Naam, sasa nitafungua ukurasa mpya. Ni mwaka mpya. Nitajaribu kufanya vizuri zaidi mwaka huu kuliko nilivyofanya mwaka jana.” Lakini, unaona, haifanyi kazi. Na ndivyo walivyo watu wanaouchukulia uponyaji wao kiholela namna hiyo; haufanyi kazi. Haidumu.

32 Lakini mwanamume au mwanamke akimjia Kristo, kwa moyo uliojitolea kabisa, na anaamini, mpaka (wao) kabisa kitu fulani kinabadilika ndani yao, mtu huyo yuna Uzima wa Milele.

33 Na ndivyo ilivyo kwa uponyaji wa Kiungu. Mtu anapomjia Kristo, juu ya msingi wa kuamini Damu iliyomwagika ya Kristo ilikuwa ni kwa ajili ya uponyaji wake, “Kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa,” na kuikubali, mpaka jambo fulani linatendeka moyoni mwake, ambalo linasema, “Ndivyo ilivyo. Nitakuwa mzima.” Ninawaambia, hakuna njia yoyote ya kuwazuia wasipate afya. Watakuwa wazima. Hiyo ni kweli.

34 Sio lazima umwambie mtu aache kutenda dhambi akisha kuzaliwa mara ya pili. Inakoma tu kabisa, yenyewe.

³⁵ Vema, ni jambo lile lile, huwaambii watu, “Sasa endelea kushikilia,” wakisha kuponywa. Wao wananinii tu...Kitu fulani kinatendeka ndani yao. Na sio nje ndani; ni ndani nje. Kinatendeka *hapa* ndani, kwanza. Unaamini kabisa. Na kisha, kutoka hapo kinatoka nje, kinaanza kufanya kazi.

³⁶ Na, basi, nimeona jambo hilo likitukia ghafla kabisa, ambalo lilisababisha miujiza ya kipekee sana.

³⁷ Sasa, kabla hatujalikaribia Neno la Mungu, juu ya somo, hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Na kila mtu, kwa njia yako mwenyewe sasa, hebu tukutane na Bwana.

³⁸ Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunakuja Kwako, kwa unyenyekevu sana, katika Jina la Bwana Yesu, Mwanao mpendwa. Tumekuja kwa Jina Lake kwa sababu ametuamuru kufanya hivyo, akisema, “Lolote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu, nitalifanya.” Basi, tukiliweka Jina Lake, tunajua ya kwamba hatuna budi kufanya mazungumzo na Mungu, nayo maombi haya yatapelekwa moja kwa moja Kwake.

³⁹ Na, Baba, tuna haja sana, leo, kujibiwa maombi haya. Nasi tunakuja, baada ya usiku wa maombi na tafakari, tukilisoma Neno, tukiuliza tu yale ambayo ungetutaka tuseme asubuhi ya leo, kwa watu wanaokufa, wagonjwa. Tukijua kwamba ni wajibu mzito sana, nasi tunapaswa kuwajibika, siku moja, kwa uaminifu wa utumishi wetu juu ya urithi wa Mungu.

⁴⁰ Basi, tunakuja Kwako kwa unyenyekevu, tukiamini, kwa mioyo iliyoinamishwa, tukisema, “Mungu, uturehemu hapa leo. Utusamehe kila dhambi, Bwana.” Jalia moyo huu, wa watu hawa hapa leo, utakaswe kabisa, hata Roho Mtakatifu atatenda kwa njia ya ajabu, akichukua Neno Lake na kuliwasilisha kwa kila moyo. Na jalia kila asiyeamini, leo, awe mtoto halisi wa Mungu, aliyezaliwa mara ya pili. Na jalia kila mgonjwa aponye leo. Roho Mtakatifu na atupe imani hiyo ya kufikia juu ambayo itapanda kupita kila uvuli na kila wingu, imshike Mungu na kumleta mbele zetu, ama au atulete katika Uwepo Wake. Tuinue juu ya vivuli. Jalia kisiwe kivuli kilichosalia. Hebu sote tuunganishe nafsi zetu na Mungu sasa.

⁴¹ Njoo kwenye Neno Lako, Bwana. Uliahidi ya kwamba utalibariki Neno Lako popote liliponenwa. Nawe ulisema halitarudi kwako bure, bali litatimiza yale liliyokusudiwa. Na, Baba, Wewe uliyelituma Neno! Sasa, naomba Roho Mtakatifu alichukue Neno sasa na kuingia moja kwa moja kwenye mioyo ya watu, na kujenga imani isiyotikisika, Bwana, ambayo itawaponya wagonjwa na wanaoteseka. Iwaokoe waliopotea. Wape tukio wale ambao hawana. Utufiche sasa nyuma ya Kristo, Bwana. Na tujalie, kunena kwetu kwote, na kuhubiri, na kushuhudia, lolote litakalotokea, yote na yawe kwa njia ya Kristo, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

⁴² Ninapowazia wema Wake! Sasa, hili ni fungu linalofahamika. Usiku kucha, nilionekana kama... Hata baada ya kwenda kulala, nisingeweza kuliondoa fungu hili mawazoni mwangu. Ilinibidi tu ku—kuliweka akilini mwangu. Ingawaje, nimeliendea mara nyingi. Nami nililiweka tu niani mwangu. Na leo hii, kwa msaada wa Mungu, nataka kuzungumza kidogo, bila kujua nini, au bila kuandaa neno moja, au chochote kile. Hatuhubiri kutoka kwa muhtasari wowote. Ni yale tu Bwana anayosema tufanye, na kuanza na kumalizia, na kujaribu kuninii, wakati... kwa amri Yake.

⁴³ Katika Kitabu cha Mwanzo, mlango wa 22 na kifungu cha 7, tunasoma hili. Kifungu cha 7 na cha 8, kwa njia ya somo tu.

Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, Babangu: naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa hiyo sadaka ya kuteketezwa?

Naye Ibrahimu akasema, Mwanangu, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka ya kuteketezwa: basi wakaendelea wote wawili pamoja.

⁴⁴ Sasa, katika kusoma Neno, kifungu kinachojulikana sana, bali nataka kuchukua kwa ajili ya somo, Mungu akipenda, kwa muda kidogo: *Mungu Anayo Njia Iliyoandaliwa.*

⁴⁵ Sasa, barabara kuu, idara ya barabara kuu, inayo barabara kuu iliyoandaliwa kwa ajili yako kuja Jeffersonville, popote unapotoka, kwa ajili ya ibada asubuhi ya leo. Ulikuwa na... Anayo barabara kuu iliyoandaliwa. Ifuate tu hiyo barabara kuu. Chukua ramani, fuata barabara kuu. Ni rahisi sana. Nenda popote nchini Marekani, kwa kuchukua tu ramani ya barabara kuu.

⁴⁶ Mungu anayo ramani iliyotiwa alama kwa ajili ya uponyaji wetu, kwa ajili ya wokovu, na ramani iliyotiwa alama kwa ajili ya Utukufu. Yote inaongoza huko. Nasi tunaposafiri kwenye barabara hii kuu ya kale, kama tukihitaji ma—mahali pa uponyaji... Utaona, kwenye ramani, kuna vituo vidogo vidogo kote kando ya barabara, ambapo Bwana ametuandalia mahali pa uponyaji. Anaohudumu kote barabarani, ambao wana... wanaamini katika uponyaji wa Kiungu, na wanawaombea wagonjwa na wahitaji.

⁴⁷ Kama yule msafiri aliyeanguka, akitoka Yeriko, kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko, wakampeleka kwenye nyumba ya wageni, mahali padogo palipoandaliwa. Nao wakamiminia mafuta kidogo, na kutoa pesa, naye akapata nafuu. Naye Bwana akasema, au huyo mtu akasema, hasa, “Kukiweko na chochote zaidi ya hiki, nitakapopitia hapa, nita—nitakilipia, nitakapopitia hapa tena, katika safari yangu ijayo.” Kwa hiyo, tunajua kwamba Mungu anayo njia iliyoandaliwa.

48 Katika tabia ya Ibrahimu, asubuhi ya leo, tukizungumza, ama tukimchukua kama wazo la msingi. Yeye, kwa maoni yangu, ni mmoja wa wahusika mashuhuri kuliko wote wa Biblia, na mmoja wa wahusika ninaopenda sana kuwaletea watu kama mfano.

49 Sasa katika Waebrania mlango wa 11, ama mlango wa 12, kifungu cha kwanza, ilisema:

...na sisi...tumezungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila dhambi, na ki—kila...uzito, na dhambi...ile ituzingayo kwa upesi,...

50 Sasa, tunatambua ya kwamba dhambi ni kitu kimoja tu, hicho ni, kutokuamini. Dhambi iko katika umoja. Dhambi... Wewe ni mwenye dhambi kwa sababu wewe ni asiyeamini. Wewe ni Mkristo kwa sababu wewe ni mwaminio. Haimaanishi, sasa, wakati mmoja, au...Mara nyingi nimesema, kwamba, kuvuta sigara, kunywa pombe, kucheza kamari, na kufanya uzinzi, kusema uongo, hiyo si dhambi. Hayo ni matokeo ya kutokuamini. Hayo ndiyo kutokuamini kunazaa. Hiyo ndiyo sababu unafanya jambo hilo, ni kwa sababu wewe ni asiyeamini. Lakini unapokuwa mwaminio, basi mambo haya yote yanatoweka, na ni maisha mapya ya imani, nayo huzaa haki, amani, furaha, upendo, uvumilivu, wema, saburi, upole. Hayo ndiyo matokeo, kwa sababu wewe ni mwaminio. Sasa, Mungu...Uliwahi kutulia ukawazia...

51 Sasa, kwa muda kidogo tu, hebu na tutazame moja kwa moja kwenye Maandiko. Nami ninayapenda, kwa sababu ni njia ya Mungu. Ni haki ya Mungu.

52 Na mambo haya yote yaliyotukia huko nyuma katika Agano la Kale yalikuwa ni mfano wa yale sisi tunayoweza kuwa kama tukichukua jambo lile lile, na barabara waliyopitia. Biblia ilisema waliokoka na makali ya upanga, walifanya mambo haya yote mbalimbali, wafu wao walifufuliwa. Nawe ulisema, "Lakini hiyo ilikuwa katika wakati wa Biblia." Hiyo inatendeka hivi leo. Huu ni wakati wa Biblia. Kwa kuwa Roho Mtakatifu amekuja, daima ni wakati wa Biblia. Kamwe hutuondoki kwake. Ingawa, mnajua tuna tahadhari juu ya mambo haya, na watu ambao hawayaamini watafanya mzaha, dhihaka. Walikuwa nayo huko nyuma, pia.

53 Lakini siku moja, maisha yatakapokwisha, hiyo hadithi itasimuliwa huko juu Utukufuni, wimbo wa ukombozi utakapoimbwa. Loo, karibu ninaweza kuona wakati Yesu atakapokuja duniani, na waliokombolewa wamesimama Mbele Zake, na mikono iliyoinuliwa, wakiimba hadithi, "Tumekombolewa kwa neema!" Wakati Malaika watakaposimama kuizunguka dunia, huku wameinamisha vichwa, bila kujua tunalozungumzia. Kamwe haikuwabidi

kukombolewa. Mimi na wewe ndio tunaohitaji kukombolewa. Mimi na wewe ndio ambao Kristo alitufia. Ndiyo sababu tunaweza kuimba “Neema ikomboayo!” Malaika hajui lolote juu yake; hakuwahi kuanguka. Huo utakuwa wakati wa jinsi gani! Loo, jamani!

⁵⁴ Ninapowazia, juu ya makunyanzi yote ya kale ya mwili huu yataondolewa; mvi zote zitatoweka; mabega yaliyoinama yatanyoshwa; “Haya, angalieni alichonifanyia.” Nena kuhusu neema ya ukombozi, mtasikia sauti yangu, najua mtasikia. Sio yangu tu, lakini ya kila mtu, utasikia sauti yao wakati watakapoimba hiyo hadithi, “Neema ya ukombozi,” jinsi alivyotukombo. Na sasa tuna sifa zake tu. Tuna malipo ya kwanza tu, arabuni yake. Siku moja tutapata malipo kamili.

⁵⁵ Yesu hakuja duniani na kufa bure tu. Yesu kamwe hakubahatisha, kuja duniani. Yesu hangefanya hivyo. Mungu hafanyi shughuli ya ofisi yake Mbinguni namna hiyo, kiholela. Yesu alikuja duniani kufa kwa kusudi fulani, na si kuona tu kama kungekuwa na mtu. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, aliweka... alitangulia kuona kitu hicho chote. Mnaamini hivyo? Alitangulia kukiona! Kwa kujua tangu zamani Yeye alitangulia kujua.

⁵⁶ Kwa hiyo, alijua ya kwamba kutakuwa na Kanisa litakaloitwa litoke, lisilo na ila wala kunyanzi. Na ilibidi yafanywe maandalizi ya kuliokoa Kanisa hilo, kwa hiyo akamtuma Yesu. Sio tu “labda mtu anaweza kuokolewa,” lakini Yeye alijua ni nani angeokolewa. Angekuwa na watu walioitwa watoke, nanyi ndio hao. Angekuwa na watu ambao wameamini katika uponyaji wa Kiungu, wangeyakubali yale mapigo kwa ajili ya uponyaji wao, nanyi ndio hao. Mungu alijua. Alijua kungekuwa na wasioamini. Walikuwako wakati huo. Alijua wangekuwako. Yeye alijua tangu zamani, kwa hiyo basi angeweza kusema awali na ingekuwa hivyo.

⁵⁷ Naye alijua tangu zamani ya kwamba kutakuwa na mtu ambaye angeli amini, kwa hiyo akamtuma Yesu kwa ajili ya wale ambao wameamini. Nao hawa hapa leo hii, wamekusanyika hapa, mahali pamoja, kukubali yale Mungu alijua tangu zamani yangetukia. Mungu alifanya maandalizi kwa ajili ya wale ambao wameamini, nanyi ni sehemu ya maandalizi hayo. Mungu alijua awali, kabla ulimwengu haujapata kuumbwa, ya kwamba siku hizi zingekuwako, hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kutabiri jambo hilo. Alijua tangu zamani, Naye akafanya maandalizi kwa ajili ya wale ambao wangelikubali.

⁵⁸ Na ninyi ndio hao watu, asubuhi ya leo, ambao mmekuja hapa kuombewa, ambao walifanyiwa hayo maandalizi. Mungu alitangulia kujua. Loo, jamani! Hilo linaamsha mhemuko wa nafsi zetu.

⁵⁹ Unapomwona Roho Mtakatifu, anapolichukua Neno na kuliweka kote katika kusanyiko, angalia mihemuko ya wasikilizaji. Mnajua ninachofanya basi? Ninajua ya kwamba Uwepo wa Mungu uko jengoni. Unapoona jinsi, matokeo, anavyowasisimua watu, unapoona Neno tu; Mungu akifanya maandalizi na kutoa.

⁶⁰ Jambo lile lile ulilolijia kwenye maskani hii, asubuhi ya leo, Mungu alilijua tangu zamani na kuliweka kwa utaratibu, ili uweze kupokea kitu kile kile ambacho umekuja kupokea asubuhi ya leo. Amina. Unalionga? Unaona, kila kitu tayari kimewekwa kwa utaratibu. Jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kulipokea sasa. Mungu tayari amelituma. Liko hapa. Sasa, jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kuinuka na kulipokea.

⁶¹ Sasa inabidi uonyeshwe jinsi ya kulipokea, jinsi ya kulifikia na kulikamata. Na kisha ukilipata, basi unajua liko. Hakuna kitakacholifutilia mbali; halifutiki. Kamwe haliwezi kubadilishwa.

⁶² Angalieni, Mungu akitupa mfano hapa, Ibrahimu na mvulana wake mdogo Isaka. Nilikuwa nikiwazia huko nyuma wakati Ibrahimu alipokuwa tu mtu wa kawaida. Hakuwa zaidi ya mwanamume mwingine yeyote. Yeye labda . . .

⁶³ Baba yake alikuwa mwabudu sanamu, aliyeshuka kwenye nchi ya Ukaldayo, na mji wa Uru, wakitoka Babeli, ambako walikuwa wameabudu mizizi ya miti. Nao walikuwa na mwanamke fulani kule juu, naye ilisemekana ni mungu fulani wa kike na kadhalika, aliyejengwa na—na Nimrodi. Na huko ndiko ibada ya sanamu ilikoanzishwa kwanza, huko Babeli. Ndipo watu wakatawanyika. Nayo Babeli ikawaleta wote katika kundi moja, kama kiongozi mmoja mkuu, ama dhehebu moja kuu.

⁶⁴ Lakini Ibrahimu alitoka katika kundi lililojiondoa; baba yake. Alikuwa amemwoa dada yake wa kambo, naye akashuka, lakini . . . na kuishi ma—mabondeni, katika bonde la Shinari. Na hapo Mungu akasema naye, akiwa na umri wa miaka sitini na- . . . au umri wa miaka sabini na mitano, na akamwahidi kisa cha uponyaji wa Kiungu. Naye mke wake, Sara, alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano. Naye akaahidi kwamba kupitia imani yake, ndani Yake, ya kwamba angemfanyia Sara uponyaji wa Kiungu. Amina.

⁶⁵ Ni picha nzuri jinsi gani! Ajabu jinsi gani! Jinsi, ambavyo huyo, kama ukiangalia, daima ilikuwa ni imani ya Ibrahimu! Hata Sara alilitilia shaka, na hata akacheka, na kubishana na Mungu Mwenyewe, jambo hilo, hata akamcheka. Lakini Mungu, kupitia ukuu Wake, asingeighairi ahadi Yake.

⁶⁶ Loo, laiti mngeweza kuona jambo hilo, enyi wagonjwa, hapo ndipo jambo fulani litakapotukia. Halina budi kutukia. Inategemea imani yako kwa Mungu.

⁶⁷ Sasa, Mungu alimwambia Ibrahimu angefanya, na kuweka njia fulani, ili hili litendeke. Yeyote hapa ambaye amepita, au popote katika umri wao wa utineja anaweza kujua, ya kwamba hilo lilipaswa kuwa la kipekee. . . ilibidi jambo fulani litokee. Lakini kabla Mungu hajafanya jambo hilo, ama kuliahidi, Yeye alifanya maandalizi yake kabla hajatoa ahadi. Na itabidi iwe.

⁶⁸ Kwa watu wanaoketi hapa asubuhi ya leo, wakiwa na kansa, shida ya moyo, vipofu; itabidi iwe ni kazi ya Kimbinguni ambayo itafanya jambo hilo.

⁶⁹ Ilibidi iwe ni kazi ya kimbinguni, Jumapili asubuhi, Jumapili iliyopita asubuhi, kumwondoa mama huyo kutoka kwenye machela iliyowekwa hapa. Vifundo vya miguu vilivyovunjika, na ugonjwa wa mchacho wa seli, hata asingeweza kujivika joho; katika dakika kumi na tano, angeweza kujizungushia. Maandalizi yalifanywa. Unaliona? Loo, ni jambo tukufu jinsi gani!

⁷⁰ Maandalizi yalifanywa. Mungu alijua tangu zamani ya kwamba angemtuma Ibrahimu, naye akamwacha ashuke moja kwa moja mpaka alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, kuonyesha ungekuwa ni mwujiza, kumwacha Sara aendelee moja kwa moja. Naye angeliweza kusema nao walipokuwa na umri wa miaka kumi na minane au ishirini, bali aliacha tu ifikie mahali ambapo ingekuwa ni mwujiza.

⁷¹ Mungu anapenda kuonyesha Nguvu Zake. Si kwamba inamlazimu; lakini anapenda kufanya hivyo. Hilo, linampendeza, katika uweza Wake, kuwafanya raia Wake wajue Yeye ni Nani. Nina furaha sana kuhusu jambo hilo, kwa sababu alinionyesha nguvu Zake. Kwa kawaida, Mungu anapoonyesha nguvu Zake, haidhuru watu wanafikiria nini kulihusu, watu watalipigia kelele kila wakati. Inatayarisha mioyo yao. Inawafanya kuwa tayari. Inawafanya wajifunge kiuno na kuwa tayari kuchukua hatua mpya.

⁷² Watu ambao hawaamini katika uponyaji wa Kiungu, na kutenda miujiza, jinsi ambavyo si ajabu makanisa yetu yanakufa. Si ajabu yananyauka yakafikia kwenye madhehebu yasiyo na Damu. Si ajabu Injili ya kijamii imesheheni sana siku hizi, ni kwa sababu katika seminari zetu, na kila kitu, tunaondoa mambo yote ya ajabu kutoka kwa Mungu.

⁷³ Naye Mungu Mwenyewe ni wa ajabu sana. Yeye Ndiye Muumbaji. Yeye ni Yehova. Yeye ndiye Ukweli mkuu. Yeye ndiye Kiini kikuu cha kila kitu kilichoumbwa juu ya nchi, kiliumbwa na Yeye. Naye anaonyesha Nguvu Zake kwa kulichomoza jua kila asubuhi, kwa kutuma mvua Yake, kwa kuweka pinde Zake za mvua. Anashuka kwa raia Wake, na kuponya magonjwa yao na kuokoa dhambi zao. Amina.

⁷⁴ Neno lenyewe, “Mungu,” Mwenyewe, neno *Mungu* linamaanisha “kitu cha kuabudiwa.” Nasi tunamwabudu

kwa sababu Yeye...Katika utukufu Wake, kwamba aliweka mambo haya mbele yetu, nasi tunayaona wazi mbele ya macho yetu. Jinsi ilivyo tukufu kumtumikia Yeye! Jinsi anavyojua mambo haya tangu zamani na kuyaweka katika utaratibu!

⁷⁵ Labda, leo, unasema, “Ndugu Branham, mimi ni Mkristo. Jambo hili lilifikaje kwangu? Kwa nini nikaingia katika hali kama hii?”

⁷⁶ Vema, labda Mungu alifanya hivyo kama tu alivyofanya kwa Ibrahimu na Sara. Mbona, Sara alikuwa ameolewa, labda, na Ibrahimu alipokuwa tu msichana tineja. Ibrahimu, pengine kijana mwenye umri wa miaka ishirini na kitu. Kulikuwa na tofauti ya miaka kumi katika umri wao. Labda mwanamke akiwa na kumi na sita naye ishirini na sita. Kwa nini angeweza kusema nao, aseme, “Sasa, mtakuwa na mtoto sasa katika ujana wenu. Mnaweza kumpenda mtoto wenu sasa wakati mngali wachanga, na mnaweza kumfurahia sana. Nanyi mtamlea, naye atakuwa mfano wa Mwokozi ajaye,” na kadhalika. Angeweza kufanya hivyo wakati huo. Lakini Mungu anapenda kufanya miujiza. Loo! Samahani. Lakini kujua yale amefanya!

⁷⁷ Nikitazama juu ya uso wa watu, ninamwona mwanamke ameketi hapa ambaye alikuwa akifa kwa kansa naye hakuwa—hakuwa chochote ila kivuli cha mwanamke, naye alikuwa tu karibu sana na kufa. Huyu hapa ameketi, asubuhi ya leo, mwenye afya, mwenye nguvu, mwenye mashavu ya kupendeza.

⁷⁸ Huyu hapa msichana kwenye kiti cha mbele. Nilikuwa tu nikizungumza naye, muda mfupi uliopita, mojawapo ya hatua mbaya sana za mlevi sugu. Naye huyu hapa, hana sura ya fadhaa; ni mpole na mnyenyekevu.

⁷⁹ Ninatazama kule nje na kumwona mwanamke huko nyuma ambaye alikuwa kipofu, naye huyu hapa asubuhi ya leo, hana hata miwani machoni mwake.

⁸⁰ Loo, ni Mungu akifanya njia, Naye aliifanyia pale Kalvari. Mle ndani, matumaini yetu hayajajengwa juu ya kitu chochote pungufu ya Damu ya Yesu na haki Yake. Loo, jinsi afanyavyo hilo! Hayachunguziki, lakini Yeye hufanya hivyo. Naye anafanya hivyo kwa ajili ya Utukufu Wake. Naye amefanya maandalizi kwa ajili yake.

⁸¹ Kama ulikuwa umpeleke mtoto wako kwenye karamu ya aina fulani, si ungemtayarisha na kuweka mavazi yake tayari, na kadhalika, ama suti yake ndogo, vyovyote alivyo huyo mtoto, mvulana ama msichana? Ungefanya maandalizi kwa ajili yake.

⁸² Kama ulitaka kukaribisha kikundi fulani, si ungeninii... kwa chakula cha jioni, si ungetayarisha chakula chako cha jioni kwanza? Kwa kuwa, unajiandaa kwa ajili ya mambo haya. Unajiandaa kwa ajili ya baraka hizi kuu zinazokuja, upate kuwapa watu. Hivi hupendi kuwakaribisha watu? Hupendi kutoka na kuwapeleka watu nyumbani kwako na

kuwakaribisha? Unasafisha kila kitu, unaandaaa kila kitu. U—unaweka ua dogo *hapa*, “Hivi ndivyo wangependa tu.” Na unarekebisha kitu kidogo *hapa*, “Sasa, naona, wao ni... Wanapenda hiki,” na kwa hivyo ungekirekebisha, ukifanya maandalizi tu. “Nami najua wanapenda aina hii ya nyama,” kwa hivyo unatayarisha nyama hiyo iwe tamu sana na ya kupendeza. Kwa sababu, na kama huwezi kujisikia kulifanya, unamleta mtu mwingine aje kulifanya, ambaye anaweza kulifanya vyema zaidi. Unafanya maandalizi, matayarisho ya jambo fulani, kwa sababu unataka mgeni wako aburudike kabisa.

⁸³ Mungu, aliyefichwa katika nyakati za kale, alitaka watoto Wake wapate kilicho bora zaidi, kwa hiyo akafanya maandalizi. Alilitanguliza kupitia kwa manabii. Alikuwa amelifunua katika Kristo. Nayo meza imeandaliwa leo. Na kila mwanamume na mwanamke ambaye amealikwa, amekaribishwa kuja kwenye Meza hii, “Kwa maana alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tulipona.” Yote yanaonekana kimbele! Kimewekwa, na kuandaliwa. Chakula kiko tayari. Wito umetolewa. Aliliona tangu zamani. Alifanya maandalizi. Ni njia iliyowekwa na Mungu kwa ajili yenu, wakati nafsi zenu zina njaa.

⁸⁴ Mama mmoja aliniambia, asubuhi ya leo tu, kasema, “Niliingia kwenye mmoja wa hiyo mikutano, nikaona watu wakiwa na furaha sana.” Kasema, “Sikuwa na furaha. Kisha nikawaangalia, nikasema, ‘Hakika walikuwa na kitu fulani. Laiti ngingekuwa na hicho.’” Hakika, Meza iliandaliwa kwa ajili ya nafsi hiyo maskini, yenye njaa. Na kabla ya ibada kwisha, alikuwa akila kwenye Meza ile ile. Loo! Kwa nini? [Dada huyo anasema, “Ndugu Branham, huyo alikuwa ni mimi.”—Mh.] Hiyo ni—hiyo ni kweli. [“Na sasa—sasa nina furaha leo.”] Amina.

⁸⁵ Mlevi, mlevi sugu mwenye macho mekundu, mlevi kupindukia, madaktari wao walikuwa wamemkatia tamaa; huyu hapa, mwenye furaha, anashangilia. Na hiyo imekuwa kama miaka miwili iliyopita, nadhani. [Dada huyo anasema, “Miaka mitatu.”—Mh.] Miaka mitatu iliyopita. Na, angalieni, bado inashikilia.

⁸⁶ Ukiwahi kuja kwenye Meza hiyo, mara moja, na kuweka miguu yako chini yake, kamwe hutaondoka tena. Ni nzuri sana! Ulimwengu hauna chochote cha kulinganisha nayo. Ni ajabu sana kujua upendo Wake kwako. Mungu, akifanya maandalizi!

⁸⁷ Sasa Yeye alisema, “Nitamwacha Ibrahimu... Na badala ya kumwita sasa, akiwa na umri wa miaka ishirini na sita, na Sara akiwa na kumi na sita, nitasubiri hata watakapozeeka. Nitaacha ipite kukoma hedhi kwa Sara. Loo, kwa kawaida hutokea kwenye yapata miaka arobaini, ndipo basi... arobaini, hamsini, sitini. Ikipita takriban miaka ishirini na mitano, ndipo

nitamwita. Na kisha nitamwacha Ibrahimu afikie sabini na mitano, ndipo nimwite.”

⁸⁸ Sasa, alisema, “Ibrahimu, nitakufanyia jambo fulani.” Hilo ni zuri vya kutosha, mradi tu Mungu alisema atafanya hivyo.

⁸⁹ Ibrahimu akasema, “Vema, Bwana, hakika nimefurahi kumpata.” Naye akaendelea akitenda kama kwamba tayari alikuwa naye. Amina. Ndivyo ilivyo. Ikiwa Mungu anayo, asingeninii. . . Asingelisema isipokuwa amelitayarisha. Ikiwa amelitayarisha, basi ni kama tu umelipata.

⁹⁰ Kama nikikwambia nitakupa mwaloni, nawe ukasema, “Vema, Ndugu Branham,” mimi huyu hapa naja na mbegu ndogo ya mwaloni na kukupa. Una mwaloni. Hakika, naam. Uko katika hali ya mbegu. Lakini iache tu, ipande ardhini, itazaa mwaloni. Bila shaka.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa Neno. Neno ni mbegu.

⁹¹ Neno lilimjia Ibrahimu. Neno la Mungu lilimjia, na kusema, “Ibrahimu, nimekuchagua wewe.” Mnalipata? Loo, ninapenda tu hilo! Sio, “Ulinichagua Mimi,” lakini, “Nilikuchagua wewe.”

⁹² Na kwa nini mko hapa, asubuhi ya leo, mlio wagonjwa? Mungu aliwachagua. Leo hii ndiyo siku yenu ya uponyaji. “Nimewachagua. Nimeandaa chakula changu cha jioni. Nimewakaribisha ndani. Sasa, kila mmoja wenu ni mgeni, na mmeingia. Nami nimetayarisha kila kitu, na vitamu vyote vimewekwa mezani, na kila mmoja wenu anaweza kuvipata sasa.” Ni mwaliko wa jinsi gani! Sasa, Mungu anasema sasa, wakati mwingine. . .

⁹³ Ibrahimu, bila shaka Ibrahimu angesema, “Asante, Bwana. Nina furaha sana kupata hii, ahadi hii ambayo umenipa. Kwa sababu, mimi hapa, mimi ni mzee, na sikuzote nimetaka watoto. Kwa hiyo, mimi ni—mimi ni mzee, na ni—ningependa kupata ahadi hiyo.”

⁹⁴ Naam, Ibrahimu aliendelea, kana kwamba aliamini kwamba mtoto huyo angezaliwa mwaka uo huo. Lakini, mnajua, siku baada ya siku, hakukuwako na mabadiliko. Na kisha ikaenda, siku baada ya siku, kisha wiki baada ya wiki, na mwaka baada ya mwaka, na hakuna mabadiliko. Lakini Biblia ilisema. . .

⁹⁵ Sasa, kama hiyo ingekuwa mimi na wewe, vema, labda. . . Sisemi mimi na wewe. Lakini watu wengine, wangesema, “Loo, jamani! Mungu, Mungu aliniaibisha. Hakutimiza ahadi Yake.” Lakini alitimiza ahadi Yake.

⁹⁶ “Naye Ibrahimu,” Biblia ilisema, “alipata nguvu katika Mungu.” Wakati wote, ilizidi kuongezeka. Sasa, yeye ana umri wa miaka sabini na mitano. Sasa miaka kumi imepita, ana miaka themanini na mitano.

⁹⁷ Miaka kumi! Hebu wazieni, hapo ndipo nilipoanza kuhubiri mikutano hii, na miaka kumi imepita; na bado hakuna

kilichotendeka, mtu wa kwanza niliyewahi kumwombea, lakini bado angekuwa akimtukuza Mungu kwa sababu ingetokea. Kwa nini? Mungu aliitayarisha.

⁹⁸ Mungu hatakupa ahadi isipokuwa kwanza kuna amana kwa ajili yake. Mtu mzuri hatakupa hundi, bila pesa kwenye benki. Mtu mwaminifu hatakupa. Vema, Mungu asingekupa hundi Yake kwa ajili ya wokovu wako, au uponyaji, isipokuwa kulikuwa na amana kwa ajili yake. Mungu ameandaa.

⁹⁹ Alimwambia Ibrahimu kwamba atampata mtoto. Hilo lilitosha.

¹⁰⁰ Alimwambia Nuhu. Alisema, “Nuhu, nataka unijengee safina. Ujenge kwa kuokoa nyumba yako; safina.” Naye Nuhu... Je, si ni nzuri, katika Mungu? Kabla ya maafa haya makubwa kutokea, Mungu daima hutoa onyo na kufanya njia ya kuepukia. Anaitayarisha. Alisema, “Sasa, ninii... Nuhu,” liangalie, “nataka ujenge safina.” Mbona, hawakuwa na maji juu ya nchi; chemchemi ndogondogo tu. Haijawahi kunyesha. Hakukuwako na mvua angani.

¹⁰¹ Na jinsi wakati mwingine inaonekana kuwa ya kipumbavu, kwa akili ya kimwili, wakati Mungu anapompa mtu ahadi, jinsi ulimwengu hauwezi kulielewa. Hapana shaka ila kwamba ulipopokea baraka za Mungu na kuzaliwa mara ya pili, wewe, watu walidhani wewe ni mwenda wazimu. Walisema, “Mtu huyo ana kasoro kidogo tu.”

¹⁰² Unaona, unatembea kwa imani. Loo, jamani! Unajitayarisha kwa kitu ambacho ulimwengu haujui chochote kukihusu. Wanaishi tu kadiri wanavyoweza kuona. Lakini tunaishi kwa mambo tusiyoona, ambayo tunaamini, ambayo Mungu alisema yalikuwa ni kweli. Imani haiangalii kitu ambacho unaweza kuona. Imani huangalia vitu usivyoviona.

¹⁰³ Jinsi tunavyopaswa kuwa na furaha asubuhi ya leo, basi, kila mtu humu ndani akijiandaa kwa ajili ya uponyaji wako. Hakika. “Je, nitafanyaje hilo? Sijui. Lakini, Mungu aliniandalia, ninakuja kupata... kuupata. Ni hayo tu. Nitakuwa vile hasa Yeye alisema nifanye, nami nitaupokea.” Mnaona? Kwa maana ndio njia iliyowekwa na Mungu ya kufanya hivyo. Anafanya maandalizi.

¹⁰⁴ Sasa, Nuhu alitoka akaenda kule na kuanza kuijenga hiyo safina. Fadhili ya Mungu kwake; alisema, “Sasa, Nuhu, janga fulani linakaribia kutukia. Na wote wasio katika safina hii watazama, kwa hiyo jitayarishe na uingie kwenye safina hii, na uingize familia yako mle. Mwambie kila mtu. Kila mtu anakaribishwa kuja, lakini nina hakika hawatakuja. Lakini wewe ninii tu—wewe fanya tu—fanya tu maandalizi kwa ajili yao, kwa vyovyote vile. Na hii hapa safina, nawe ujenge safina hii. Na kila mtu anayetaka kuingia, anaweza kuingia na kuokolewa.” Basi Nuhu akaenda zake, akijenga.

¹⁰⁵ Kama wewe ulivyo, leo, ukiendelea kujenga ushuhuda wako. Unajenga safina ya kiroho, kwa ajili ya kuokolewa kwa nafsi yako, kwa ajili ya ushuhuda wako, na kwa utukufu wa Mungu.

¹⁰⁶ Sasa wanaendelea kuijenga safina, nao watu wanapitia hapo na kumcheka na kumdhihaki. Nao wanasema, "Aisee, ulisikia kuhusu yule jamaa akisema maji yatashuka? Kwani yatatoka wapi? Mbona, hakuwezi kuwa na maji huko juu. Angalieni, hivi mnaweza kuona maji yoyote? Ni bluu tu iwezavyo kuwa. Vema, tumeishi hapa miaka hii yote, hakujawahi kuwa na maji. Yangewezaje kuja? Hakuna maji huko juu, na jamaa huyu anasema, 'Dunia nzima itafunikwa na maji.' Vema, mtu huyo hapana shaka kuwa kidogo ni wa kuchekecha tu hapa juu. Ana kasoro kichwani mwake."

¹⁰⁷ Lakini kwa nini alifanya hivyo? Kwa nini akafanya maandalizi? Kukidhi maandalizi ya Mungu? Mungu alikuwa anaenda kujiandaa kuwaangamiza maadui wa dunia, naye Nuhu ikambidi kutengeneza njia ya kutayarisha kitu cha kuendeshea kupita hayo.

¹⁰⁸ Na hivyo ndivyo ilivyo leo. Mungu amefanya njia ya kuiangamiza hiyo kansa. Mungu amefanya njia ya kuondoa upofu kutoka kwa hayo macho. Mungu amefanya njia. Nasi tunajaribu kufanya nini na Neno hili, asubuhi ya leo? Je, ni kujenga kitu cha wewe kuendesha, kuufikia ushindi wako. Neno la Mungu, BWANA ASEMA HIVI, unaona, kupitia kwenye Neno Lake. "Mungu alisema hivyo!"

¹⁰⁹ Baada ya kitambo kidogo, wakati Mungu alipokuwa tayari kwa jambo hilo kutokea, mvua ilikuwa juu kule. Na Mungu atakapokuwa tayari kwa jambo hilo kutukia, litakuwepo daima. Mnaona? Mungu hufanya njia Yake, baada ya kufanya maandalizi. Vema.

¹¹⁰ Alifanya jambo lile lile, alitaka kujitukuza Mwenyewe katika wana wa Kiebrania. Akafanya maandalizi. Aliyafanya lini? Wana wa Kiebrania hawakuwa na ahadi yoyote. Wasingeweza kurudi hapa na kusoma katika Biblia, na kusema, "Bwana, uliahidi katika Neno Lako ya kwamba yeyote wa watoto Wako akipata kuingia katika tanuru ya moto, ungewakomboa. Vema, Bwana, tunakuja moja kwa moja juu ya jambo hilo." Naam, hilo lisingekuwa ngumu sana kufanya; imani yao tu, kwa sababu Mungu alikuwa ameliahidi tayari. Lakini Mungu hakuwa amewaahidi kitu kama hicho.

¹¹¹ Lakini, haya hapa maneno waliyokuwa nayo. Mungu alikuwa halisi sana kwao; walisema, "Mungu wetu anaweza." Vipi kuhusu hilo, jamaa ambaye haamini katika uponyaji wa Kiungu? "Mungu anaweza kutukomboa, tanuru hii ya moto na ije, lakini hatutazisujudia sanamu zako." Basi walipoingia kwenye tanuru ya moto, wakiwa na imani tupu, halisi, ya kwamba Mungu aliweza; hawakuahidiwa, bali aliweza. Mungu

akamtuma Kristo kwenye hiyo tanuru ya moto, na kuupeperusha huo moto kutoka kwao, na kuwalinda na kuwatoa nje. Hakika. Lakini, nasema, Mungu anaweza.

¹¹² Sasa huji, ukisema, “Mungu anaweza.” Sio lazima uje hivyo.

¹¹³ “Mungu, uliahidi! Amina! Uliitayarisha pale Kalvari, nami nimekuja kuipokea. Ni maandalizi Yako. Uliiandaa. Nawe uliahidi, nami ninaona wengine wakiipokea, kwa hiyo mimi naja, pia, Bwana, kupata sehemu yangu ya hiyo.” Utaondoka mtu tofauti. Utaondoka ukiwa na uthabiti kama huo ndani ya nafsi yako, hata hakuna kitu kinachoweza kukufadhaisha. Unajua kwamba umeponywa. Unajua kwamba Mungu ameshughulikia jambo hili kwa ajili yako, kwa sababu ameahidi.

¹¹⁴ Yeye hutoa majaribio na vipimo pamoja na ahadi hizi. Yeye, mara nyingi, alifanya hivyo.

¹¹⁵ Na kuwaacha wana wa Kiebrania wahisi uzito wote wa moto ukija juu yao.

¹¹⁶ Alimwacha Danieli asikie mngurumo wa simba, na labda pumzi yake yenye joto moja kwa moja dhidi yake. Simba hao, wakiwa wamefungua vinywa vyao, wana njaa, chini kwenye shimo hili. Ndipo hao simba wakamkimbilia moja kwa moja, na kwa kishindo kikuu na mlipuko mkuu, hata wakawa tayari kumkamata Danieli. Mara moja, alifunikwa na Malaika. Amina! Nuru ikamzunguka Danieli. Bila shaka ilikuwa ni ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli.

¹¹⁷ Wanyama wanaogopa moto. Mnajua hilo. Wanaogopa sana mwanga. Unaweza kuumulika uso wa mnyama yeyote, naye atatoroka.

¹¹⁸ Na labda Mungu alimulika, maana Mungu anaishi katika mwangaza. Mungu ni Moto ulao. Na labda, kwa ghafla, bila kujua, alisema, kitakachotokea. Lakini wakamtupa katika tundu la simba. Ndipo Roho Mtakatifu alikuwa pale, nao simba wakarudi nyuma na kulala chini. Ilikuwaaje?

¹¹⁹ Si ajabu, Mtakatifu Agnamu, alipokuwa anakufa, alipoufikia ule msalaba nao walikuwa wanataka kumwua. Basi aliukimbilia huo, akaukumbatia msalaba na kuubusu, ambao wangeupaka lami na kumtia manyoya. Naye akasema, “Ee msalaba wa Kristo, nasikitika tu kwamba nilikuwa na uhai mmoja tu ninaoweza kutoa kwa ajili Yako. Nasikitika tu kwamba nilikuwa na uhai mmoja tu ninaoweza kutoa kwa ajili Yako.”

Wakasema, “Hivi unaogopa?”

¹²⁰ Akasema, “Ati kuogopa?” Nao wakaifunga mikono yake msalabani, wakamlowanisha kwa lami, kisha wakamfunika kwa manyoya, wakaweka pipa la lami chini yake. Kisha wakapitia hapo, katika gari la farasi, na kutupa mwenge uliowashwa ndani

ya mwali wa moto, nao ukamzunguka. Ndipo baada ya watu kushangilia na kupitisha mawe yao, wao kwa wao, kwamba wamemwondoa mdudu huyu, mhubiri wa haki, ilikuwaje? Huo moto ukazima, naye huyo mtakatifu alikuwa aking'inia msalabani, akimsifu na kumtukuza Mungu. Mungu alikuwa ameandaa njia ya kuepukia kwa ajili yake, katikati ya huo moto. Alikuwa ameandaa njia. Kwa nini? Alikuwa kwa ujasiri, kwa ushujaa.

¹²¹ Hivyo ndivyo tunavyokuja kwenye ahadi za Mungu. Tunakuja kwa ujasiri kuzikubali. Hatuji, tukitetemeka, tukisema, “Labda nitapata. Labda mimi. . . Jumapili ijayo, labda *hili* litakuwa *lile*.” La. Tunakuja tukiwa na uhakika moyoni mwetu, tukisema, “Mungu, kupitia kwa Kristo, ameitarisha njia, na nimekuja kuikubali.” Ni jambo rahisi unapoangalia na kuona ni nani aliyetoa hiyo ahadi, kama ukiona ya kwamba ni Mungu aliyetoa hiyo ahadi. Kama Mungu alitoa ahadi, Mungu anaweza kutimiza ahadi Yake.

¹²² Wakati yule mama mzee mcha Mungu, Jumapili iliyopita, akiwa amelala pale, nami nikasema, “Mama, unaamini kwamba Mungu atatimiza ahadi Yake?”

¹²³ Akasema, “Kwa moyo wangu wote.” Loo, jamani! Hiyo ilikuwa ndiyo. Hiyo ndiyo iliyolifanya.

¹²⁴ Hilo ndilo lililolifanya, hapa si muda mrefu uliopita, nikisimama huko Karlsruhe, Ujerumani, wakati mvulana wangu na mtu fulani walipokuwa wakiwapanga watu kwenye mstari wa maombi. Akaja msichana mdogo, kipofu, Mjerumani. Alikuwa kipofu kabisa. Wala sikujua shida ya huyo mtoto. Walimpandisha tu juu. Maskini huyo mtoto alikuwa akitoka jukwaani; mtu mmoja akamnyakua. Naye alikuwa na mawimbi-wimbi madogo, nyuzi za nywele zilizoning'inia chini, zimesokotwa; msichana wa kawaida tu, mdogo, Mjerumani; hajawahi kuona, maishani mwake mwote. Nao walipomleta pale, kamwe hakujua pa kwenda. Naye akanikumbatia. Licha ya hayo, nikiwa nimevaa suti ii hii, niliyo nayo. Akanikumbatia kwa maskini mikono yake midogo. Akanong'oneza kitu fulani katika Kijerumani; sikujua ni nini. Mkalimani akasema. . . Nikasema, “Alisema nini?”

¹²⁵ Kasema, “Alisema, ‘Je, wewe ndiye ndugu atakayeniombea?’” Loo, jamani! Mtoto mdogo namna *hii*, kama mtoto wangu Rebekah.

¹²⁶ Nami nikasema, “Naam, kipenzi. Nimekuja kutoka huko mbali Marekani, kukuombea.” Akaweka ninii yake midogo. . . akanikumbatia kwa mikono yake midogo, akakilaza maskini kichwa chake juu ya bega langu. Hakikisho tu, urahisi wa watoto, Mungu wa Mbinguni alikuwa atatenda kazi, kwa njia fulani.

¹²⁷ Dakika chache, akafungua macho yake madogo. Akasema, “Ni . . . Mnaviitaje vitu vile?”

“Taa.”

¹²⁸ Mama yake akaruka na kupiga mayowe, na kuvua viatu vyake, akakimbilia jukwaani. Akasema, “Kipenzi!”

Akasema, “Mama, kumbe wewe ni mrembo sana.”

¹²⁹ Kwa nini? Kalvari ilijiandaa, ikafanya maandalizi kwa ajili ya uponyaji wa macho yake. Bila shaka. Alikuwa kukubali kile ambacho Mungu alikuwa ameandaa.

¹³⁰ Mungu alimwandalia kila mmoja. Mungu hutoa hakikisho. Labda ugonjwa wako umekuwa wa kukawia. Labda umekuwa nao kwa miaka mingi, nawe umejaribu na kujaribu. Ulijaribu.

¹³¹ Ibrahimu alijaribu. Alipokuwa amefikia, karibu umri wa miaka mia moja, Mungu alimtokea siku moja. Naye akasema, “Ibrahimu, Mimi ni Mungu Mwenyezi. Uende mbele yangu ukawe mkamilifu.” Umri wa miaka mia moja, kwenye mia moja hasa. “Uende mbele Yangu ukawe mkamilifu. Mimi ni Mungu Mwenyezi.” Na ikiwa ungeyachambua maneno hayo . . .

¹³² Wakati mwingine, labda, ningependa kufanya uamsho maskanini, ama hapa Jeffersonville, tutakapoweka hema letu na kadhalika, ambapo tunaweza kuyachukua maneno hayo na kuyachambua, tuone kile yanamaanisha, maana tu za maneno hayo.

¹³³ Mwenyezi, kwa Kiebrania, ni *El Shadai*, ambalo linamaanisha, “titi,” kama mwanamke. “Ibrahimu, ninakuja kwako kwa jina la Mwenye Matiti, Muuguzi, M—Mpaji-Uhai.”

¹³⁴ Kama mtoto mchanga akiwa mgonjwa, mwajua, mama yake humshikilia kwenye titi lake na humnyonyesha. Naye mtoto huyo mchanga anahangaika na kulia, na amekonda sana, bali analala tu pale na kunyonya, na kupata nguvu. Nanayonya uhai wake kutoka wapi? Kutoka kwa mama.

¹³⁵ Naye Mungu anatutokea leo, kama *El Shadai*, Mwenye Matiti; yote mawili, Agano Jipya na la Kale, yaliyojaa ahadi tu kadri yawezavyo kuwa. Sio titi; lakini, “mwenye matiti,” mawili. Kwa nini? Alikufa kwa madhumuni ambatani. Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake, Mungu aliandaa njia kwa ajili ya uponyaji wetu. Mnaona? Moja kwa ajili ya wokovu wetu; moja kwa ajili ya uponyaji wetu. “Mimi ni Mwenye Matiti. Nina mashahidi wawili. Kwa vinywa vya mashahidi wawili kila neno na lithibitishwe.”

¹³⁶ Katika Agano la Kale, Yeye alikuwa *Yehova-yire*, “dhabihu ya Bwana iliyotolewa.” Alikuwa *Yehova-rafa*, “Bwana akuponyaye.” Katika Agano la Kale, katika majina Yake ambatani, Yeye alikuwa mponyaji, wa *Yehova-rafa*.

¹³⁷ Katika Agano Jipya, Yeye ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Yale Maandalizi. Tungeweza kulichukua kutoka katika Agano la Kale au Jipya, tuyabandike pamoja. Hiyo ndiyo sababu, mara nyingi, mimi huenda kwenye Agano la Kale, kuchukua somo, kwa sababu ninalileta katika Agano Jipya, na kulivuta pamoja na kuwaonyesha, ni Mungu yeye yule mwenye matiti.

¹³⁸ Yeye yule aliyemwepushia Danieli mauti, kwa kumtuma Malaika, ni Mungu yeye yule aliye humu ndani asubuhi ya leo. Ni Mungu yeye yule, aliyeyafungua macho ya kipofu Bartimayo, aliyemponya msichana huyo mdogo Mjerumani. Yeye hashindwi kamwe. Yeye ni Mungu, Yehova. Hawezi. Anafanya maandalizi. Naye ameandaa njia kwa kila mmoja wetu. Ameandaa njia ya kuepukia.

¹³⁹ Naye akamwambia Ibrahimu, “Mimi ni Mwenye Matiti. Sasa, Ibrahimu, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuendelea tu kunyonya, kunyonya.”

¹⁴⁰ Basi angalieni mtoto mchanga, akiwa mgonjwa, haidhuru ni mgonjwa jinsi gani. Sasa, kwa akina mama, lijueni jambo hili. Hata huyo mtoto mdogo awe mgonjwa kiasi gani, maadamu ananyonya, ameridhika. Na wakati mwingine unamwandalia maziwa yake kidogo, kama anatumia chu—chupa, nawe unayatayarisha maziwa yake kidogo na kutia vitamini ndani yake.

¹⁴¹ Loo, jinsi linavyopendeza! Mnajua, labda sisi sote ni watoto wachanga wa chupa wa Mungu, labda tungenema. Naye Mungu alikuwa ameandaa chupa mbili tu, Agano Jipya na la Kale, Naye akatia tu vitamini zote ndani ya chupa hizo. Nasi tunapomshika, tukaanza kunyonya, si kwamba tu tunaridhika, bali tunaponywa, yote kwa wakati ule ule. Tuna vitamini za kiroho. Zinaendelea tu kutujenga, kutupa nguvu zaidi, na nguvu zaidi. Ni nzuri. Zina kalisi kwa ajili ya mifupa. Naam. Zina vitamini B changamano kwa ajili ya mishipa. Loo, ina kila kitu ndani yake. Kabati zima la dawa za Mungu lilitiwa ndani yake. Zote zilikuwa kwenye chupa, ziliwekwa kwenye chupa, Naye akaifungulia pale Kalvari.

¹⁴² Kwa hiyo, kupitia Kalvari, tunaweza kulishwa baraka zozote zilizokombolewa ambazo Yesu alifia. Mkuki, ukiwakilisha dhambi ya mahali petu, uliuchoma ubavu Wake, miguu Yake, mikono Yake, kichwa Chake. Na, kupitia kuvuja kwa uhai Wake, tunalishwa tupate Uzima, tena, yote tuliypoteza katika kule kuanguka kule nyuma. Mungu ametuandalia njia. Mungu ameandaa njia ya kuepukia.

¹⁴³ Sasa, huyu hapa mtoto Isaka, alipozaliwa, baada ya Ibrahimu kufikia umri wa miaka mia moja; naye Sara alikuwa karibu umri wa miaka mia moja, takriban miaka tisini. Ndipo Mungu akamleta mtoto Isaka. Ndipo mtoto Isaka akazaliwa.

Na alipozaliwa, vema, jinsi hiyo familia ilivyofurahi! Walifanya karamu siku ile aliyochishwa maziwa. Ibrahimu alimtahiri baada ya siku nane. Na huyu hapa anakuwa kijana sasa, wa miaka kumi na sita hivi. Mungu akasema, “Sasa, Ibrahimu, ninataka kuona kweli una kiasi gani cha imani. Nitakupa pingamizi katika uponyaji wako wa Kiungu, nione ni umbali gani utakaoniamini Mimi.”

¹⁴⁴ Unajua, wakati mwingine una pingamizi. Je, ulijua hilo? Nimekuwa nazo chungu nzima. Naam, nimekuwa nikihubiri Injili kwa miaka mingi; nikabadilika, nikawa mgonjwa sana, sijui la kufanya wakati mwingine, lakini nanga yangu inashikilia. Amina. Itie tu nanga karibu na Kalvari, na useme, “Mungu! Loo, siwezi kuona Kalvari. Mawimbi ni mazito sana! Watu wangu wanasema *haya* yote. Daktari anasema siwezi kuishi. Lakini, Kitu fulani *hapa* ndani, kamba Okozi ingali inashikilia.” Kushikilia!

¹⁴⁵ Uliwahi kuona meli ikiwa na wavu wa kukokota, bahari . . . wavu wa baharini, hasa? Itapita kwenye mawimbi.

¹⁴⁶ Wakati mwingine tuko chini ya mawimbi; huwezi kuona karibu nawe, au popote. Lakini acha nanga yako ishikilie tu hapo. Itakuweka, nanga inapoanza kushikilia. Na katika magonjwa na kadhalika, Mungu basi anayatoa yote vyema. Hatimaye anga zinakuwa shwari. Kila kitu kinakuwa sawa. Inashikilia ndani ya pazia.

¹⁴⁷ Alisema, “Sasa nitakupa majaribio, Ibrahimu.” Akasema, “Nataka umchukue huyu kijana wako wa miaka kumi na sita. Nataka umpeleke huko nje, Nami nataka umwue sasa.”

¹⁴⁸ “Nitakuwaje baba wa mataifa? Ambapo, kutoka kwa mvulana huyu, atatokea je Kristo? Basi itakuwaje nikimwua?” Vema, sasa, anawazia, “Ikiwa Mungu alifanya hiyo ahadi, ni juu ya Mungu kushughulikia hayo mengine.”

¹⁴⁹ Kwa hiyo, anamchukua huyo mvulana mdogo. Asingemwambia mama. Ndipo anafanya sa—safari ya siku tatu huko nyuma jangwani. Sasa, mtu anaweza kutembea kama maili ishirini na tano, thelathini kwa siku, kwa hiyo hapana shaka alikuwa maili mia moja kutoka kwenye ustaarabu. Ndipo akaona mlima kwa mbali sana. Akawaambia wa—wale waliokuwa wamewashika nyumbu, akasema, “Ninyi kaeni hapa.” Sasa, ninawatakeni mwangalie jambo hili, ninyi watu ambao ni wagonjwa. Kasema, “Ninyi kaeni hapa wakati mimi na huyu mvulana tukienda kule mlimani na kuabudu, nasi tutarudi. Tutarudi.” Vipi . . .

¹⁵⁰ “Atarudi vipi, kama unampeleka kule juu ukamwue? Naye Mungu alikwambia umwue, maneno waziwazi ya ‘kuutwaa uhai wake,’ nawe utautoa uhai wake, mtarudi vipi?” Hiyo ni juu ya Mungu. Loo, jamani! Hamwezi kuliona? Labda ni mimi tu, kimhemuko asubuhi ya leo. Mnaona? Je, atarudi vipi?

Lakini, Mungu akamwambia Ibrahimu, “Nenda ukafanye hivyo.”

¹⁵¹ Ibrahimu akasema, “Nilimpokea kama mtu kutoka kwa wafu. Na kama nikimwua, Mungu anaweza kumfufua tena. Mungu alitoa ahadi kwamba yeye, kupitia kwake, Mwokozi angekuja, na kwa namna fulani Mungu atafanya hivyo.”

¹⁵² Musa. Baba na mama yake Musa iliwabidi kufanya kitu kama hicho. Musa atakuwaje, kuwakomboa watu, walipoona alikuwa mtoto mzuri, kama wakimtia huko nje katikati ya kundi la mamba? Atakuwaje m—mkombozi? Atafanyaje jambo hilo? Vema, walimpokea kwa njia hiyo, kwa hiyo wakamsukuma huko ndani kwenye mamba, wakijua kuwa Mungu angeweza kumshughulikia. Naye Mungu kweli alimshughulikia.

¹⁵³ Mungu ameweka mkono Wake juu ya Kanisa Lake. Mungu ameweka mkono Wake juu ya mwanamume Wake, juu ya mwanamke Wake. Mungu ana uwezo wa kushughulikia hali hiyo.

Kwa hiyo, Ibrahimu akasema, “Tutarudi.”

¹⁵⁴ Hivi ulipotoka nyumbani asubuhi ya leo, ulimwambia mumeo, “Nitakaporudi, nitakuwa nikijisikia tofauti”? Naam, bwana.

“Utajuaje jambo hilo?”

“Sijui; lakini nitakuwa.” Loo! Amina!

¹⁵⁵ “Nitakuwa tofauti nitakaporudi. Wewe angalia tu uone.”

“Utafanyaje jambo hilo?”

“Mungu atajalia.”

¹⁵⁶ Hapo, wakati saa hii kuu, muhimu sana ilipofika, nao wakapanda juu ya kilele cha mlima. Ndipo Ibrahimu akachomoa kisu chake, akamchukua huyo mvulana mdogo. Naye akamwambia swali hili, akasema, “Baba, hizi hapa ku—kuni, na hii hapa madhabahu, lakini iko wapi sadaka ya kuteketezwa?”

Akasema, “Mungu ataleta sadaka.”

¹⁵⁷ Je, hilo si ni somo kwetu? Mungu ataleta. Hakuna haja ya sisi kufadhaishwa na chochote. Mungu ataleta.

¹⁵⁸ Ninakazia macho kitu fulani sasa hivi, lakini kinaweza kuniharibu na kuniangamiza. Sasa, mlinisikia nikiingia, kutoka kwenye ibada; nikaenda kufanya kazi na Ndugu Wood kule nyuma. Lakini Mungu akashuka, siku chache zilizopita usiku, katika ono, na kuniambia na kunionyesha la kufanya. Ukimtumaini tu, Yeye ni wa ajabu sana. Anajua yote. Atakupita kilicho bora zaidi kilichopo.

¹⁵⁹ Niliitazama Pontiaki yangu ya kale hivi majuzi, inachakaa sana sasa. Haidromatiki inaisha, kwake. Nami nina wasichana wawili wadogo wanaorukaruka sana, vitini, nao karibu wavunje

hivyo viti, kutoka kwake. Nami nikaenda na kuvipeleka vikafanyiwe ukarabati. Naye huyo mtu akasema, “Billy, nitakambia nitakalofanya,” kasema, “nitakupa badilisho zuri kwa ajili ya hivyo.”

Nikasema, “Ninawezaje kuvibadilisha hivyo?” Nikasema, “Siwezi kufanya hivyo.”

¹⁶⁰ Akasema, “Vema, wewe ni... Loo, mkopo wako ni mzuri hapa, maadamu unautaka. Nitashikilia barua yako.”

Nikasema, “Hilo ni zuri sana, lakini siwezi kufanya hivyo.”

¹⁶¹ Kasema, “Nitakupa bei nzuri sana kwake.” Kasema, “Kwa kuwa u mhubiri, nitakupa kwa bei ya jumla.”

Nikasema, “Hiyo ni sawa, lakini, unaona, si—siwezi kufanya hivyo.” Mnaona?

¹⁶² Naye akasema, “Vema, kama ukifikiria kukibadilisha, nijulishe.”

Nami nikasema, “Vema.”

¹⁶³ Hivyo basi nikawazia, “Vema, Mungu, mimi... Kitu hiki cha kale ni sawa kwangu. Ni kizuri kabisa, hicho ni lori langu la zamani.” Nikasema, “Tunaweza kwenda kote, nchini kote, nalo. Ni sawa. Nimekuwa nikifanya hivyo miaka hii yote; naweza kuendelea.”

¹⁶⁴ Ndipo hivi majuzi usiku, simu ikaja kutoka California. Halafu mtu mmoja akanipigia simu, mtu ambaye ni milionea mara nyingi. Akasema, “Ndugu Branham, una gari la aina gani?”

Nami nikasema, “Nina Pontiaki ya miaka minne.”

¹⁶⁵ Akasema, “Tarehe thelathini na moja ya mwezi huu, kutakuwako na mojawapo ya Kadilaki kubwa sana, zilizotengenezwa, italetwa na kuwekwa mlangoni pako, kwa ajili ya matumizi yako.”

¹⁶⁶ Nikasema, “La. Usifanye hivyo, ndugu. Tafadhali.” Nikasema, “Usifanye hivyo.” Nikasema, “Kama... Usifanye hivyo.” Nikasema, “Majirani zangu wasingeelewa hilo, na watu. Sihitaji Kadilaki yoyote.” Nikasema, “Chukua iliyobaki na umpe mtu fulani. Na kama unataka kunisaidia, ninunulie Ford, vema, ama Chevi,” nikasema.

¹⁶⁷ Akasema, “La, hii tayari imenunuliwa, na iko hapa.” Sijui nitafanya nini nayo.

¹⁶⁸ Lakini, unaona kile kilicho, ni Mungu. Mungu, katika rehema Zake, akileta. Wakati mwingine kitu fulani hudorora sana, ambapo tunashangaa itakuwaje, lakini Mungu tayari ametoa. Anakishikilia tu hapa juu, akipata riba kwacho, mnaona, apate kukupa.

¹⁶⁹ Na kwa ono, sasa ninayumbayumba huko nje. Hii hapa barua inakuja, ikitoka kule, kwa mtu fulani, hivi majuzi. Ilitumwa, imetumwa kwangu sasa, ya mfalme wa taifa, kwe—kwenye

nchi za ng'ambo. Naye akasema, "Loo, miujiza na kadhalika, imetukia katika Ujerumani!" Mfalme wa Denmaki, alisema, "Njoo huku, Ndugu Branham, ukawahudumie watu wangu, katika Jina la Bwana Yesu." Na papo hapo wakati nilipowazia Mungu alikuwa amenifagilia mbali, na nilikuwa nimekwisha, Yeye anaweka upya. Haleluya!

¹⁷⁰ Halafu basi, wakati, ilikuwa inanibidi kuwachukua watu kwa upambanuzi, mmoja mmoja. Ameweka moyoni mwangu sasa jambo ambalo nisingethubutu kulizungumzia kwa wakati huu. Wala mimi si mlokole, nanyi mnajua hilo; hakika mnanifahamu vizuri vya kutosha. Lakini angalieni kinachotukia sasa. Loo, jamani! Itakuwa mbali zaidi. Mnaona?

¹⁷¹ Wakati mwingine katika wakati wenye giza kabisa, ndipo Mungu anaingia. Haleluya! Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo.

¹⁷² Hivyo ndivyo Mungu alivyomfanyia yule mwanamke mwenye kutokwa na damu. Saa yake iliyo na giza sana, ndipo Yesu akaja.

¹⁷³ Ilikuwa ni saa ya giza sana ya wana wa Kiebrania, ndipo Mungu akaingia kwa pepo za wakati, na kuupuliza moto ukawaondokea wana wa Kiebrania.

¹⁷⁴ Ilikuwa katika saa ya giza sana kwa Ibrahimu, alipokitwaa kile kisu, na kumlaza mvulana wake mwenyewe nyuma, na kukivuta kichwa chake nyuma; huku moyo wake ukiwa kinywani mwake, tuseme. Mwanawe mwenyewe, naye akakitwaa kisu, ili kukata koo lake, kwa sababu Mungu alikuwa amesema hivyo. Yalikuwa ni majira yenye giza kuliko yote, wakati Mungu, Yehova, alipojitokeza jukwaani. Kasema, "Ibrahimu, ondoa mkono wako. Nimeleta, tayari."

"Ati umefanya nini?"

"Nimeleta, tayari, dhabihu."

¹⁷⁵ Ibrahimu akasema, "Nitapaita mahali hapa Yehova-yire, kwa kuwa Bwana ametoa."

¹⁷⁶ Na yapata wakati huo, kondoo dume akaanza kulia nyikani, amenaswa, huku pembe zake zimenaswa katika matawi fulani. Kondoo huyo alitoka wapi? Yuko maili mia moja kutoka kwenye ustaarabu. Wanyama, simba, na mbwa mwitu, na kadhalika, na fisi, waliokuwa wakizunguka-zunguka malishoni huko, wangelimwua. Isitoshe, yeye yuko moja kwa moja juu ya mlima, ambako hakuna maji, hakuna chemchemi, hakuna chakula chochote kwake kula. Mara, huyu hapa kondoo dume amenaswa nyikani, kwa pembe zake.

¹⁷⁷ Ilikuwa ni nini? Yehova, Mungu, alinena huyo kondoo-dume akatokea. Hakika, alimnena. Halikuwa ono. Alimwua huyo kondoo dume. Damu ikamtoka. Ilikuwa ni kondoo dume halisi. Hakika, alikuwa. Nayo damu ikamtoka. Naye hu—huyo kondoo dume akawa, dakika moja, na kuondoka katika dakika

iliyofuata. Ilikuwa ni njia ya Mungu iliyoandaliwa kutoa baraka kwa mtoto Wake ambaye alikuwa amemwamini hadi mwisho wa safari.

¹⁷⁸ Mungu anaweza, katika dakika hii, kunena kila kansa kutoka kwenye jengo hili, kufungua kila jicho lililopofuka, angeweza kumweka kila mtu huru, anayemwamini. Mungu anayo njia iliyoandaliwa. Ameandaa njia. Alimtuma Mwanawe, Kristo Yesu, naye Roho Mtakatifu anaatamia juu yetu leo hii. Roho Mtakatifu yuko juu yetu. Anatubariki. Analeta mazingira.

¹⁷⁹ Ni kwa nini unaweza kuchukua yai la kuku na kuliweka kwenye nyumba ya kuatamia? Mama kuku si lazima awe juu ya hilo yai, lipate kuanguliwa. Ni kwamba tu liwe na joto juu yake, litaanguliwa.

¹⁸⁰ Loo, Mungu, Yeye alituma Neno Lake. Na hilo ndilo ninalojaribu kuwapa, Neno Lake, ahadi Yake. Aliiandaa pale Kalvari. Alitayarisha dhabihu kwa ajili ya uponyaji wako asubuhi ya leo. Anayo hapa. Naye huiangalia. Nawe unaipata moyoni mwako, naye Roho Mtakatifu anaiatamia. Itapata Uhai na kuzaa vile hasa Mungu alisema ingezaa. Kila Neno litazaa kile hasa lilichoahidi, maana Mungu ameliweka.

¹⁸¹ Angalieni yale maandalizi. Wakati mtu anapojiandaa kuweka ninii wao...kuweka kuku wao na kadhalika, jinsi wanavyochagua mayai yao na kuyaweka chini ya kiatamizi, na kuyaweka katika nyumba ya kuatamia, na jinsi joto linavyodhibitiwa. Joto hilo huwekwa juu ya yai hilo hata litakapoanguliwa.

¹⁸² Naye Mungu ameweka utaratibu sana, kwamba siku moja...Kupitia mifano yote, huko nyuma kupitia kwa Adamu, kupitia kwa Hawa, na kuendelea kupitia kwa manabii, hadi kupitia kwa Ibrahimu, Yeye aliweka utaratibu. Aliyaweka yote katika Agano la Kale, akionyesha yale ambayo alikuwa anaenda kufanya.

¹⁸³ Naye akamalizia pale Kalvari, alipomtuma Yesu, "Aliyejeruhiwa kwa makosa yetu; akachubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu juu Yake; kwa kupigwa Kwake sisi tulipona." Aliimalizia pale Kalvari.

¹⁸⁴ Ndipo akawapaka mafuta wahubiri na kumtuma, sasa, kuleta Neno, na kuweka mayai mahali pazuri, kuyaweka. Ndipo Yeye huchukua Neno lili hili na kuliimarisha huko nje, kisha anakuja na kuzunguka-zunguka juu Yake, kwa Roho Mtakatifu, mpaka Neno hilo linakuwa Uzima katika moyo wa mwanadamu, na pepo wote kutoka kuzimu hawangeweza kuuzuilia Uzima. Naam, bwana. La, la.

¹⁸⁵ Hata hilo yai liwe nini! Ikiwa ni yai la bata, litaleta bata. Ikiwa ni kuku, litaleta kuku. Ikiwa ni ndege, litaleta ndege.

¹⁸⁶ Kama Mungu aliahidi wokovu, uweke moyoni mwako. Roho Mtakatifu ataataamia juu yake mpaka utakapopata Uhai. Kama aliahidi uponyaji, uweke moyoni mwako. Ni njia ya Mungu iliyoandaliwa.

¹⁸⁷ Alituma ishara na maajabu. Alisema, “Katika siku za mwisho, itakuwa, asema Mungu. Loo, nitamtuma Roho Wangu Mtakatifu ulimwenguni. Kisha nitawatuma wahudumu. Na ishara kuu na maajabu yatatokea. Kwa Jina Langu watatoa pepo wachafu. Nao watanena kwa lugha mpya; wakishika nyoka, au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

¹⁸⁸ Nayo Biblia ilisema, “Katika siku hii ya mwisho, kutakuja mvua ya masika na ya vuli, pamoja.” Na, siku hizi, kote katika mataifa, kutoka kwa wale... mashariki hadi magharibi, kutoka kaskazini hadi kusini, ni uamsho mmoja mkuu unaodumu, wa uponyaji wa Kiungu, Nguvu za Mungu. Na mtu aliyetupwa chini, mtu ambaye ameokotwa... Mungu alijaribu kuingiza katika makanisa haya makubwa, wala asingeweza kupata nafasi. Waliukataa na kusema usingewezekana, wakati ulipowaziwa, hapa miaka michache iliyopita.

¹⁸⁹ Lakini Mungu akashuka chini katika njia duni ya maisha, watu duni, maskini, akawainua, wasio na elimu. Kwa nini Mungu akafanya hivyo? Loo, kama ungalipitia katika makanisa makubwa na kadhalika, wangekuwa na kitu cha kujitukuzia. “Vikundi vye—vyetu vilikutana pamoja. Tukaamua hivi.” Lakini Mungu aliwashukia wanaume na wanawake ambao hawawezi kusoma majina yao wenyewe wakati mwingine. Mungu huchukua kitu duni, na kufanya kitu fulani kutoka kwacho, nao walijisalimisha. Basi Mungu aliwachukua watu wa aina hiyo, akawainua ulimwenguni. Na, leo hii, mngurumo wa baraka, mpaka hata madaktari wanaliandika kwenye magazeti, kwamba uponyaji wa Kiungu ni wa kweli. Inabidi wautambue. Upo mbele ya uso wao. Haleluya!

¹⁹⁰ Tunaishi katika siku za Kuja kwa Bwana. Usiku unaingia kasi. Wahudumu wanatokwa na jasho, wanaomba; Mungu akionyesha ishara na maajabu. Lakini kuna dhoruba inayokuja. Loo, Yeye, Yeye yuaja. Kuna dhoruba inayoendelea, na wakati mkuu wa uamsho; wakati ambao ulimwengu huu haujawahi kuona, wakati kama unaopitia hivi sasa. Hakujawahi kuwa na wakati katika historia ya ulimwengu, katika wakati wowote au kipindi chochote, ambapo Injili ya Uweza wa Mungu imewahi kudhihirishwa kama ilivyo sasa hivi; kupitia redio, kupitia televisheni, kupitia wahudumu waaminifu; kuingia kwenye huduma za kimishenari, kwa Wahotentoti, kwa Waafrika, pia, kuingia Uchina, kuingia sehemu mbalimbali. Miamsho mikuu ya uponyaji, na nguvu, na matendo, na ishara, na maajabu, yanakuja kila mahali. Haujawahi kuwa hivyo, katika ulimwengu

wote, kama huo! Enyi marafiki, Mungu ameandaa. Mungu ameunena. Mungu anaufanya.

¹⁹¹ Mungu yuko hapa asubuhi ya leo. Ameandaa asubuhi ya leo kwa ajili yako. Siku hii ni siku yako. Wakati huu ni wakati wako. Ikiwa unataka na uko tayari, asubuhi ya leo, ikiwa unaamini kwa moyo wako wote! Ikiwa utamwahidi Mungu, “Mungu, si—sitacheza nalo tena. Ninakuja pekee... Kitu fulani kinatukia moyoni mwangu. Kitu fulani kidogo kilitukia hapa asubuhi ya leo. Tulipokuwa tukihubiri na kulileta Neno, sehemu hii yake ilimaanisha mimi.” Ninapooni ninii. . .

¹⁹² “Aliviita vile vitu, ambavyo havikuwepo, kana kwamba vilikuwako.” Ibrahimu alizunguka-zunguka, akisema, “Tutakuwa *hivi*. Itakuwa *hivi*. Tutampata mtoto.”

“Utampataje?” Ninii. . .

¹⁹³ “Mke wangu amezeeka kupita kiasi. Daktari anasema haiwezekani. Vema, mimi... Tutampata, maana Mungu amesema hivyo.” Basi alipoukabili ule wakati muhimu sana wa mwisho, kule juu, alipaita mahali hapo, *Yehova-yire*, “Bwana atajipatia Mwenyewe dhabihu hii.”

¹⁹⁴ Baadhi yenu mmekuja kutoka mbali sana, kuja hapa, mkifa. Simu zenu zimeandikwa pale kwenye kijidaftari kidogo, kitabu kidogo, nyumbani. Baadhi yao wana kansa. Wengine, vipofu; wengine, viziwi; wengine, bubu; wengine, baba wakiwa na watoto wachanga; na akina mama, na kadhalika, pamoja na watoto wadogo, ambao wako katika hali ya kila namna. Ni nini kimetokea? Ni nini kilikufanya ufanye hivyo? Ni nini hufanya mihemuko ya mwanadamu kuwa hivyo? Ulifanyaje jambo kama hilo?

¹⁹⁵ “Loo, tuliwapeleka hospitalini. Tulikuwa nao kila mahali.”

¹⁹⁶ Lakini kwa nini mkawaleta hapa, wakati huu? Kwa sababu kitu Fulani moyoni mwenu kilianza kutembea. Ni nini? Mungu, akitengeneza njia. Mungu, akiandaa. Maandalizi ya Mungu. Mungu ataandaa njia.

¹⁹⁷ Wengi wenu mlisikia ile hadithi ndogo ya oposamu. Ilikuwa katika vitabu, hapa si muda mrefu uliopita. Ikiwa Mungu alimjali vya kutosha maskini oposamu mjinga; isitoshe, bali nyakati zingine ilikuwa ni wanyama ninaowafahamu. Unasema, “Je, ungechukua muda kumwomba mnyama?” Kama Mungu akimtuma, naam, hakika. Mungu ni Yehova. Yeye hufanya kazi tu kwa njia Yake Mwenyewe, nasi tunamtumikia tu. Sisi ni watumishi Wake.

¹⁹⁸ Na sasa, ndugu yangu, dada, Mungu ameandaa njia kamili kwa ajili ya uponyaji wako asubuhi ya leo.

¹⁹⁹ Je, unajua kwamba nilikuwa karibu kipofu, wakati mmoja? Ilibidi niongozwe kwa mikono yangu. Nilivaa miwani mikubwa na minene machoni mwangu. Na kichwa changu kilitetemeka

hivi, na nisingeweza hata kunyolewa mtu asije akakishika kichwa changu. Fred Montgomery, hapa chini kwenye Barabara ya Sita, kwenu ninyi watu mlio na... Wengi wenu mmemjua Fred Montgomery, yule kinyozi hapa chini. Ni mara ngapi nimeweka miwani yangu chini; Fred anashika kichwa changu kwa mkono mmoja, akijaribu kukata nywele zangu kwa huo mwingine; nao unatetemeka hivyo. Nisingeweza kuona nipate kutembea. Ningeshuka kupitia mitaa ya Louisville, wakati mwingine ninakuwa kipofu sana, ingenibidi tu kufuata njia yangu kando ya ua, namna *hii*. Nami ningesimama na kungoja kidogo, macho yangu yafumbuke; mwenye wasiwasi sana.

Loo, neema ya ajabu! Leo, jinsi Yeye alivyo mtukufu kwangu!

²⁰⁰ Najua wakati Mayo Brothers kule juu waliposema, “Mbona, Bw. Branham, huwezi kuishi.” Kasema, “Mbona, haiwezekani kwako kupata... kupona huo.” Kasema, “Ninii—ninii... Huwezi kabisa.” Akasema, “Hiyo ni, hiyo hapo, inahusika katika nafsi yako.” Naye akasema, “Hakuna mtu anayeweza kupata utendaji wa nishati ambazo hupitia kwenye huo mshipa, ambao ndio nafsi yako, na kuumba niani mwako.” Kasema, “Haiwezekani.” Kasema, “Tuna maelfu ya magonjwa kama hayo yanayoletwa hapa.” Kasema, “Hakuna jambo tunaloweza kuwafanyia.” Kasema, “Huna matumaini, bwana. Ninachukia kukwambia hivyo.” Loo, jamani!

Nilipotoka nje, nilisema, “Huduma yangu imekwisha.”

²⁰¹ Ndipo Yesu akaja na ono, kasema, “Usihofu. Niko pamoja nawe. Niko pamoja nawe.”

²⁰² Akasema, “Kama ungeishi, ungekuwa kijitu kidogo chembamba tu chenye uzito wa takriban pauni mia moja na kumi, kumi na tano, karibu ulivyo sasa, labda ishirini.”

²⁰³ Nami huyu hapa, asubuhi ya leo, mia moja na sabini, ninajisikia vizuri. Ni nini? Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliye hai, alifanya maandalizi pale Kalvari, nami nikayakubali. Kwa nini akafanya hivyo? Si kwa sababu yangu, lakini kwa sababu ngingeweza kuwaambia, asubuhi ya leo, nanyi mnaweza kukubali jambo lile lile na kumwambia mtu mwingine kulihusu. Inaendelea tu. Na hiyo ndiyo njia aliyo nayo ya kuitengeneza njia, kuieneza Injili Yake. Je, mnaamini hivyo, leo? Mungu ameweka.

Na tuombe, kwa muda kidogo tu sasa, huku tumeinamisha vichwa vyetu.

²⁰⁴ Na kama dada, mpiga kinanda, kama atakuja hapa kwa muda kidogo. Nataka utoe sauti polepole:

Tabibu mkuu yu karibu sasa,
Yesu mwenye huruma;

Ananena ili kuuchangamsha moyo wenye
huzuni,
Hakuna jina jingine ila Yesu.

²⁰⁵ Sasa ninyi mlio hapa, mlio nje ya Kristo, wala hamumjui kama Mwokozi wa kibinafsi, kamwe hamjamkubali. Kuna *jambo lingine* asubuhi ya leo, kumekuwa na kitu Fulani kwenye moyo wako. Huku kila kichwa kimeinamishwa. Kitu fulani, kinachouzunguka moyo wako, kikisema, “Unajua, kitu Fulani kinaniambia tu, a—afadhali nijiandae. Siku hiyo kuu inakuja hivi karibuni sana, na mimi—mimi sina budi kusimama. Na sasa, Bwana, si kwa Ndugu Branham, bali Kwako, nitainua mkono wangu, na kusema, ‘Kwa . . . Iwapo utanisaidia, kuanzia leo hii ni—ninaenda ku—ni—nitakutumikia Wewe, tangu leo.’”

²⁰⁶ Je, kuna mtu angefanya hivyo? Inua mkono wako, useme, “Kwa neema ya Mungu, tangu leo, nitamtumikia Mungu.” Mtu fulani humu jengoni, sijui. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Hilo ni zuri. “Tangu leo na kuendelea, ninataka kuyafanya maisha yangu kuwa ya thamani kwa Bwana.”

²⁰⁷ “Mimi ni Mkristo, tayari nimemkubali Kristo, lakini najisikia kwamba nataka kuwa Mkristo bora sasa. Nataka kuinua mkono wangu na kusema, ‘Mungu, kwa hili nataka . . .’” Mungu akubariki. Loo, hilo ni zuri sana. Hilo ni zuri sana. Mungu awe pamoja nanyi.

²⁰⁸ Sasa ni wangapi, huku mmeinamisha vichwa vyenu, ambao ni wagonjwa? Semeni, “Mungu Mpendwa, sasa, nitakukubali sasa hivi. Ni—nina . . . Nina uvimbe. Nina kansa. Nina mtoto mgonjwa hapa. Nina . . .” Chochote kile, haidhuru kuna shida gani. “Nina shida fulani. Unajua. Na sasa hivi ninalikubali Neno hili, Neno Lako, kama tu nilivyokuwa nikija kwa imani kuokolewa. Ninaamini, moyoni mwangu. Kweli ninaamini, Mungu, kwamba, sasa hivi Neno Lako limetia nanga moyoni mwangu na nitapata afya. Sijui, sikuliwazia muda mfupi uliopita, lakini ni—ni—nililiamini tu sasa hivi. Nitapona sasa hivi. Nitainua mkono wangu, kukufanya ujue ya kwamba ninaamini kwa moyo wangu wote. Nitapona.” Waweza kuinua mkono wako, wewe ambaye ni mgonjwa? Loo, jamani!

²⁰⁹ Angalieni tu hiyo mikono, Mpendwa Baba wa Mbinguni! Unaona mkono wao.

²¹⁰ Ni kama tu kuongoka. Sasa, kama walikuwa wameongoka, Bwana, na walikuwa wameinua mikono yao kwa ajili ya wokovu, tungewaleta hapa kwenye kidimbwi na kuwabatiza; hilo ndilo jambo letu linalofuata. Petro alisema, “Tubuni, mkabatizwe, kila mmoja wenu, kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu; mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Sasa, hivyo ndivyo tungefanya, Bwana.

²¹¹ Sasa hawa wote waliinua mikono yao, na kusema, wanaamini ya kwamba umepanda moyoni mwao. Waliona

ya kwamba Wewe ulijiandaa kwa ajili ya uponyaji wao, tayari. Nao wako tayari kuupokea, na wanaukubali moyoni mwao. Na, Baba, kuna jambo moja lililosalia kwetu kufanya, hilo ni, kuwaleta huko na kuwaombea maombi ya imani. Kuwawekea mikono, ulisema, “Watapona.” Hakuna kinachoweza kuuzuia.

²¹² Pia, Baba, tunaamini, ya kwamba kwa neema ya Mungu, kwamba utatutumia mkutano wa uponyaji sasa ambao utakuwa wa utukufu tu. Tayari wameukubali. Tutashukuru. Tutakupa sifa. Nasi tutakupa utukufu wote. Tutawaambia wengine. Tutaenda kwenye makazi yetu, tukitoa ushuhuda. Wengine hapa wanakufa, kwa kansa; wengine hapa ambao hawawezi kuona, kutembea; wengine hawawezi kutembea. Loo, wako katika hali za kila namna, Bwana. Lakini, Wewe uko hapa ili kunyoosha kila njia iliypotoka. Uko hapa kuondoa maafa yote na kuingiza utukufu.

²¹³ Bwana, wanajifanya tupu, nami ninajifanya tupu. Tujaze, Bwana, na Roho Mtakatifu. Tujaze na baraka Zako, hata hii itakuwa siku mpya. Naomba uingie kwenye tanuru ya moto kwa wakati huu tu, peperusha mawimbi yote kutoka kwa watoto Wako, na uwakomboa kwa usalama. Tujalie, Bwana, kupitia kwa matayarisho Yako ya Yesu Kristo pale Kalvari. Tunaomba katika Jina Lake. Amina.

Tabibu mkuu yu karibu sasa,
Yesu mwenye huruma;
Ananena ili kuuchangamsha moyo wenye
huzuni,
Loo, isikilizeni Sauti ya Yesu.

²¹⁴ Enyi marafiki, wakati wakicheza, na muziki huu unaendelea.

²¹⁵ Sasa, huu ni wakati mzuri sana wa maisha yangu. Huu ni wakati mzuri sana kwangu. Ninajisikia tu nina matumaini, na kuhakikishiwa moyoni mwangu, ya kwamba Mungu atawaponya watu asubuhi ya leo, ninaposimama hapa kwenye jukwaa hili. Ninaamini hilo tu. Na hii inanifanya kujisikia... Kweli, nawaambia, nafikiri tayari imefanyika. Jambo pekee, ninaenda tu kuwawekea mikono, maana Yeye alisema tufanye hivyo; kama tu ubatizo wa maji au kitu kingine chochote.

²¹⁶ Sasa hili hapa jambo linalonipa matumaini. Ninakuja na namna hii ya matumaini kwa ajili yenu. Mnaona? Ninajua ya kwamba Yeye alinituma kufanya hili. Mimi—mimi... Nikiwa na Biblia yangu juu ya moyo wangu, na kama kamwe singeishi kutokea pale mlangoni, najua Yeye alinituma kuwaombea watu Wake. Najua hilo. Siwezi kuwaponya watu Wake, kwa kuwa tayari amefanya hivyo; hiyo imewekwa. Lakini alinituma kuwaombea watu Wake na kuwatia moyo kuamini hivyo.

²¹⁷ Sasa hebu niwaonyeshe kama ni kweli au la. Mnaona? Hebu kwanza tuchukue njia ya Mungu kwa ajili yake. Hebu

tuangalie duniani kote, ni makumi mangapi ya maelfu ya viwete, vipofu, vilema, waliopooza, waliojaa kansa, na kila kitu, ambao wameponywa. Sasa, hiyo ni ya kwanza. Baada ya Neno Lake kusema angelifanya, basi Yeye huyu hapa anakuja na kulithibitisha.

²¹⁸ Jambo lingine, kunao watu wanaoketi papa hapa, ambao wameponywa, bila shaka. Mnaona? Hao ni wa pili.

²¹⁹ Halafu hebu tuangalie tena, moja kwa moja kwenye wakati ule, miaka kadhaa iliyopita. Kuna wachache waliosalia hapa maskanini, labda, asubuhi ya leo. Baadhi yao hawaji tunapokuwa na ibada ya uponyaji, kwa sababu ya umati wa watu kusukumana namna hii. Lakini, angalieni. Papa hapa, papa hapa Jeffersonville, kwenu ninyi watu wa nje, ndipo ile Nurur, ile Nyota ya Asubuhi, ilipoonekana kwanza. Papa hapa imetukia, kwenye jukwaa hili, mara nyingi, papa hapa.

²²⁰ Bila shaka, watu walifikiri ilikuwa ni ya ulokole, lakini ulimwengu wa kisayansi umeipiga picha na kusema, “Ni ukweli.” Basi, nimewaambia ukweli. Hiyo ni kweli? Na sasa yote yamekwisha. . .

²²¹ Sasa waliipiga huko Ujerumani, hapa hivi majuzi. Nyote mlima picha za hiyo. Kamera kubwa ya Kijerumani ilitaka kuona kama wangeweza kuipiga, kwa hiyo wakaja, wakaiandaa picha. Wakati iliposhuka, basi walianza kufingirisha kitu hiki kikubwa hapa na kupiga picha hiyo, na hapo ilionyesha ikishuka kutoka Mbinguni.

²²² Wakati uvuvio ulipokuja; ikaonyesha mtu huyo aliyekuwa amesimama pale ni nani, ikamwambia juu ya kile alichokuwa, na kile kilichokuwa kimetukia, jinsi alivyokuwa akiongoza kundi la wakomunisti, na kadhalika. Kasema, “Wewe si Mjerumani, kwa vyovyote vile. Wewe ni Mwitaliano.” Ikamwambia hivyo.

²²³ Nao, yule Mjerumani pale, akipiga picha yake hivi, na kuipiga upesi, kisha anageuza kamera yake ya kufingirisha, akiipiga haraka namna hiyo. Na hii hapa imetokea; ikiionyesha ikishuka, ikiionyesha ilipokuwa kwenye upako, na kuionyesha ikiondoka, ikitoka nje ya hilo jengo. Hiyo ni kweli. Ushahidi, ni ukweli. Mnaona? Ni kwa ajili ya nini? Ni kwa ajili yako, kwa ajili yako.

²²⁴ Na, hebu wazia, chini katika ulimwengu wa wanyama, jinsi Mungu atakavyofanya, na ule usahili wake. Ungeweza kumwazia mtu fulani. . . Watu wengi hucheka hilo. Wakristo hawalicheki. Lakini hivi unajua Mungu anajua kila shomoro mdogo aliyeko? Je, unajua Yeye amehesabu kila unyoya katika bawa lao? Anajua yote kumhusu. Alisema, “Hakuna hata mmoja wao angeweza kuanguka chini bila Baba kujua hilo.” Anajua alipo kila mnyama mdogo. Anajua kila sehemu mdogo kukuhusu wewe. Anajua yote juu yake. Na kwa kufanya hivyo, unaona, na kunihakikishia. . .

225 Na kumalizia yote, ilikuja hivi majuzi usiku, aliponionyesha, nikisimama pale kando ya ziwa hili. Sitasahau kamwe.

226 Mtaliona kwenye magazeti. Nitayaleta hapa kwa ajili yenu. Mtayaona katika *Sauti ya Uponyaji*, hayo magazeti mengine.

227 Jinsi nilivyoona hilo, kwa mvuto huo mara moja, Naye akasema, “Hapo ndipo ulipojua magonjwa yote ya watu, wakati wao... kwa mikono yao.”

228 Na kisha mvuto wake wa pili. Kasema, “Kwa nini uliivuta kwa nguvu hivi? Kwa nini ulijaribu kuelezea yote hayo?” Kasema, “Unaona, ulimkamata samaki tu, lakini alikuwa mdogo.”

229 Akasema, “Sasa tupa chambo chako ndani, kwa wakati huu.” Kasema, “Weka ndoano yako.” Nikaona hiyo Nuru ikienda, ikitoka namna hiyo, kasema, “Nitakutana nawe.” Loo, jamani! Ninajua. Ninajua tu. Wakati mimi... Zaidi ya ninavyojua mimi... Ni—ninajua ya kwamba niko hai, nikisimama kwenye mimbara hii asubuhi ya leo, ninajua.

230 Ondoa tu imani yako *hapa* juu sasa, na uiweke *hapa* chini, useme, “Mungu Mpendwa, naja, nikijua, pia. Ninakuja nikijua. Naja Kwako, nami nitaponywa asubuhi ya leo.” Kama mwanadamu, ninaweza kukuombea.

Unasema, “Je, maombi hufanya lolote? Ma—maombi yatasaidia?”

231 Bila shaka, ndivyo tunavyopaswa kufanya. Maombi... Maombi hubadilisha mambo. “Maombi ya imani humwoko mgonjwa huyo.” Hiyo ni kweli? Wengine wamewekwa Kanisani kuwaombea wagonjwa. Wengine wamewekwa Kanisani kutabiri. Wengine wamewekwa Kanisani kuhubiri, wengine kufundisha. Hiyo ni kweli? Bila shaka. Tumewekwa kwa ajili ya mambo haya.

232 Kwa hiyo, nilijua kwamba nililetwa humu ulimwenguni kuwaombea wagonjwa. Nisingeweza kuwaombea watoto wote wa Mungu walio wagonjwa, nilipoanza kule nyuma, wakati kila kitu kilikuwa kimekufa, na miaka michache iliyopita. Lakini, Mungu aliwainua kutoka kwenye huduma hii, Oral Roberts na, loo, mamia ya wengine, kote. Wakaingia Afrika, huko walikuwa na uamsho mkubwa. Wakaenda katika nchi zingine, huko walikuwa na uamsho mkubwa. Watu wa Mungu kila mahali, wakifanya kazi pamoja, si kupingana wenyewe kwa wenyewe. Wote kwa pamoja, kama kitengo kimoja kikubwa, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, wakijaribu kuwafanya watoto Wake kuwa na afya njema, na kuwaonyesha Utukufu wa Bwana Yesu Kristo. Kulingana na Neno Lake, Yeye ameahidi jambo hilo.

233 Walikuwa wakijaribu kutushambulia na kubishana nasi, wahubiri ambao hawakuamini katika uponyaji wa Kiungu. Husikii mengi juu yake tena. Sivyo? Hiyo ni kweli. Iliwafichua

tu na kuonyesha walijua Maandiko kiasi gani. Na ndipo Mungu akaja tu na kuithibitisha kazi hiyo, kwa ishara zikifuata, na hilo latosha tu.

²³⁴ Sasa, ni wangapi walio hapa leo, watu wa nje ya mji, ambao wako nje ya hili jimbo mahali fulani, wanaotaka kuombewa, naomba uinue mkono wako. Hebu tuwaache waje kwanza, watu walio nje ya jimbo, halafu, watu walio nje ya mji; na kisha wale ja—jamaa, wafuate, wanaotoka hapa nyumbani.

²³⁵ Sasa, watu wa nje ya jimbo waje kwanza, madhabahuni. Hatuna nafasi nyingi hapa. Lakini naamini kama mngefanya tu, kama ndugu huyu hapa, kwa namna fulani mpange mstari, moja kwa moja namna hiyo. Kisha wanaotoka nje ya jimbo, na ndipo tutajaribu kuwapata hao. Na halafu wanaofuata, tu—tutawachukua wanaotoka nje ya... nje ya mji, halafu wanaofuata ni jamaa wa humu mjini. Pageni tu mstari kwa ajili ya maombi. Sasa...

Sasa, *Amini Tu*.

²³⁶ Sasa kuna wengi wamesimama. Baadhi yenu, bila shaka, wanakuja, labda, pengine kuona kile Bwana wetu atafanya. Angalieni muone anachofanya. Hatuogopi. Tunajua atakachofanya. Yeye atalifanya Neno hilo kuwa halisi jinsi liwezavyo kuwa. Naam, bwana. Mtaona atakachofanya. Atawaponya wagonjwa na wanaoteseka. Atawaponya, kwa Nguvu Zake na kwa utukufu Wake.

²³⁷ Sasa nitawauliza ikiwa mtanifanyia jambo fulani. Jambo la kwanza, nataka kila mmoja wenu awe na hakikisho kamili, imani, inayoamini ya kwamba Mungu atawaponya wagonjwa hawa katika mstari huu.

²³⁸ Sasa, ni wa kutoka nje ya jimbo. Wao si wa Indiana. Wanatoka katika jimbo lingine. Tuna furaha kuwa pamoja nao hapa, asubuhi ya leo, imani yao katika Mungu.

²³⁹ Sasa, ni wangapi wenu wanaoamini ya kwamba Mungu atawafanya... Ninyi watu wa jimbo sasa, wanaamini ya kwamba Mungu atawaponya, inueni mikono yenu. Semeneni, "Ninaamini, tunaamini kwa moyo wetu wote."

Sasa tuko hapa kuwasaidia, marafiki wapendwa.

²⁴⁰ [Ndugu mmoja anasema, "Ndugu Branham...?... hali ambayo hawawezi kumfikisha jukwaani."—Mh.] Nitamwombea. Nitashuka nimwendee, basi.

²⁴¹ Vema. Ninawatakeni ninyi watu wapendwa hapa, ambao mmetoka nje—kutoka nje ya hili jimbo, kuamini hili sasa. Nakutaka uamini kwa moyo wako wote, kwamba mimi... Kwamba Yesu Kristo ni maandalizi ya Mungu kwa ajili ya uponyaji wako, kwamba Mungu alimleta Yesu ulimwenguni kwa ajili ya uponyaji wako.

²⁴² Sasa, kumbukeni, hakuna kitu ndani yangu, ambacho ningeweza kufanya kuwaponya. Lakini jambo pekee ninalofanya, ninafuata amri ambayo Mungu alinipa, kulifanya hivyo. Na kujua...Mmesikia mikutano, jinsi kila kitu kimefanyika. Bila shaka, Yeye atafanya hivyo. Atafanya hivyo asubuhi ya leo kwa ajili yenu, nanyi mnaweza kurudi kwenye jimbo lenu mnalolipenda, mkishangilia tu na kuwaambia watu mambo mema ambayo Mungu amefanya.

²⁴³ Sasa, viwete wanatembea, vipofu wanaona, viziwi wanasikia, bubu wanazungumza, mambo hayo yako tu katika Uweza wa Mungu kuyafanya. Sasa nataka ninyi nyote mwamini kwa moyo wenu wote. Sasa, jambo pekee ninalopaswa kufanya, ninapaswa kuomba na kuwawekea mikono, nikiomba maombi ya imani. Nanyi hamna budi kuyakubali kwa misingi hiyo, ya Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo, na Mungu atawafanyia hayo mengine. Unaamini hilo sasa, kwa moyo wako wote? Uko tayari kuupokea. Amini ndani ya moyo wako. Neno, kwanza, liko moyoni mwako, kulifanya. Vema.

²⁴⁴ Sasa nataka kila mtu atulie kabisa, au kwa namna fulani avumishe tu, chochote unachotaka kufanya, huku tukiomba kikusanyiko. Ndipo, mmoja baada ya mwingine, naye Ndugu Neville atawapaka mafuta, wanapokuja kwangu kuombewa. Vema.

²⁴⁵ Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu, kila mahali. Na kila dakika chache tutakufanya uinue kichwa chako.

²⁴⁶ Sasa, Baba wa Mbinguni, tunakushukuru, asubuhi ya leo, kwa ajili ya Yesu. Na hapa panasimama, katika mstari huu hapa asubuhi ya leo, magonjwa mbalimbali. Unajua hayo ni yapi; sijui. Lakini, kadiri nijuavyo, Bwana, nilijaribu kuwaambia ya kwamba Wewe umeandaa uponyaji wao tayari. Baadhi yao wanaweza kuwa siku chache tu kufikia mauti. Lakini, Baba, maombi hubadilisha mambo. Hezekia aliomba, baada ya Wewe (Mungu) kumtuma nabii Wako kule na kumwambia atakufa; lakini aliomba, Nawe ukayahifadhi maisha yake.

²⁴⁷ Sasa, Bwana, ninaomba kwa moyo wangu wote, kwa ajili ya watu hawa, ya kwamba utayahifadhi maisha yao, kwa kusudi moja, Bwana, kwa utukufu Wako, hata watawaambia wengine, ndipo hao wengine waweze kuwaambia wengine. Siku ya Bwana imekaribia, na lazima tuharakishe. Nasi tunajua Injili hii haina budi kuhubiriwa kila mahali.

²⁴⁸ Na utusaidie, leo, sasa. Na uwatie mafuta watumishi Wako hapa. Paka mafuta jengo hili upya na kwa kilindi sasa. Jalia huyo Malaika mkuu wa Mungu aingie ndani sasa kwa nguvu nyingi. Atembee moja kwa moja mistarini, bila kuonekana, hata hivyo tujue Yeye yuko hapa. Nami naomba ya kwamba utamponya kila mtu, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁴⁹ Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kila mtu, polepole sasa, *Amini Tu*, polepole sana, wakati sisi...Ndugu Neville anawapaka mafuta wagonjwa, nao wananiletea.

Amini...

²⁵⁰ [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]...?... Kila mtu awe na kicho sasa. Huyu hapa mtu mwenye kigugumizi, anagogota maneno. Naye anataka kuhubiri Neno la Mungu. Anataka kukombolewa ili aweze kuhubiri Neno la Mungu. Ninawatakeni muwe na uchaji, na kuamini ya kwamba Mungu ataondoa roho hii ya kigugumizi kutoka kwa mtu huyu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

²⁵¹ Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, nikisimama hapa katika maskani hii ndogo, iliyojengwa ovyo ovyo, hata hivyo, tukijua ya kwamba Utukufu wa Shekina wa Mungu Yule aliyekaa chini ya mbawa zilizounganishwa za Makerubi upo umesimama sasa. Na kwa kuwa nafsi zetu zinaweza kuachilia mambo machafu ya ulimwenguni yanayoenda Uweponi Mwake, nasi tunaweza kuhisi na kujua ya kwamba Yeye amesimama hapa, tunakuja kwa ujasiri, tukijua kwamba tungeninii...tukijua haya, ya kuwa tungekufa kama isingekuwa kwa utukufu wa Kristo sasa, bali Damu Yake iliyomwagika hufanya njia. Tungeweza kuja, basi, kwa ujasiri hadi kwenye Kiti Chako cha Enzi, chini ya mbawa zilizounganishwa za msalaba.

²⁵² Mungu, mtu huyu hapa, mwenye sura nzuri, mkubwa, anayeonekana shupavu aliyesimama hapa, akitaka kuhubiri Injili. Ni jambo tukufu jinsi gani! Na hata hivyo, Shetani amempa sauti ya kigugumizi, ya kugogota maneno. Bali anataka kuondoka, leo hii, apate kuihubiri Injili. Ee Mungu wa Milele, tunajua kwamba Wewe umetumia, nyakati zilizopita, vigugumizi na wenye kugogota maneno. Lakini mtu huyu anataka kuwa huru, kwa maana kinamwaibisha. Kwa hiyo, leo hii, kwa ustahilifu wa Bwana Yesu, kwa mpango wa Mungu na njia iliyoandaliwa, kwa ushuhuda wa Roho Mtakatifu na Uwepo wa Mungu, na kama mtumishi Wake, ninaweka mikono juu yake na ninaikemea roho hii. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia imwache ndugu yangu. Na jalia jambo hili ovi liondoke, ambalo lingezuia Injili. Na jalia aende na aweze kuhubiri Injili, kwa sauti yenye mlio wa kweli, inayovuma, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

²⁵³ Bwana, ninaweka hii, mikono yangu, juu yake, kwa maana ni agizo Lako. Ni agizo Lako kufanya hivyo. Kupitia kwa Yesu Kristo, kwamba utujalie, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

²⁵⁴ Nataka kila kichwa kiinamishwe, na mtu yeyote msiinue vichwa vyenu hadi msikie nikisema hivyo, tafadhalini.

²⁵⁵ Roho Mtakatifu, mponye ndugu huyu hapa, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya Utukufu wa Mungu na Injili.

Nami nakuhukumu, wewe mwovu. Ondoka, katika Jina la Yesu.

²⁵⁶ Sasa, ndugu yangu, ninaamini ya kwamba utahubiri Injili. Ninaamini. Na ninaamini kwamba utafanya hivyo bila kigugumizi, bila kugogota maneno. Nataka useme, “Bwana asifiwe.” [Ndugu huyo anasema, “Bwana asifiwe.”—Mh.] “Haleluya.” [“Haleluya.”] Haya basi. “Nampenda Bwana.” [“Nampenda Bwana.”] “Ninampa sifa.” [“Ninampa sifa.”]

²⁵⁷ Unaona, tofauti sasa. [Ndugu huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Sasa nataka... Hiyo ndiyo sababu nataka kuzungumza nawe kwa muda kidogo. Unajisikia vizuri sasa, unajisikia tofauti. Hakika, kwa sababu Bwana ame—amekujalia hili, kitu hicho kimeondoka, naam hiyo ni kweli. [“Amina.”] Hivi ni...

²⁵⁸ Sema hivi, “Nampenda Yesu.” [Ndugu huyo anasema, “Nampenda Yesu.”—Mh.] “Mungu asifiwe.” [“Mungu asifiwe.”] Siamini kuwa kitakuja tena.

Sasa endeleeni tu kuinamisha vichwa vyenu. Msikilizeni mtu huyu.

²⁵⁹ “Nampenda Yesu.” [Ndugu huyo anasema, “Nampenda Yesu.”—Mh.] “Mungu asifiwe.” [“Mungu asifiwe.”] “Nitahubiri Injili.” [“Nitahubiri Injili.”]

²⁶⁰ Hakuna kigugumizi hata kidogo. Ameponywa. Mungu akubariki, ndugu. Nenda zako sasa, ukishangilia.

²⁶¹ Sasa hebu tuinue vichwa vyetu na kumpa Mungu sifa, semeni, “Asante, Bwana Yesu.” [Kusanyiko linasema, “Asante, Bwana Yesu.”—Mh.] Huyo hapo mtu akiingia kwenye huduma, kuhubiri Injili, ambaye hapo awali alikuwa anagogota maneno.

²⁶² Musa alisema nini? “Mimi nina ulimi mzito. Nina kigugumizi cha midomo,” na kadhalika.

Mungu akasema, “Ni nani aliyeumba midomo ya mwanadamu?”

²⁶³ Unaamini sasa? Kuwa na imani sasa.

²⁶⁴ Naomba mwinamishe vichwa vyenu tena, kwa ajili ya mtu mwingine. Kila mtu katika maombi sasa. Iweni na kicho.

²⁶⁵ Sasa, shida yako, dada? [Dada huyo anasema, “Nina shida na ubavu wangu; wasiwasi.”—Mh.] Unatoka wapi, dada? [“Hamilton.”] Hamilton, Ohio. Unaamini unaenda nyumbani ukiwa mzima? [“Ndiyo, ninaamini.”]

²⁶⁶ Sasa, mama huyo ana shida ubavuni mwake, naye ametoka Hamilton, Ohio. Na ana wasiwasi sana. Huenda kusiwe na jambo lolote litakalotukia ambalo ungeweza kuona, lakini Mungu atafanya vivyo hivyo. Maumivu yatamwacha, naamini; kama utaamini, pamoja nami.

267 Sasa, Baba mpendwa wa Mbinguni, nikitambua ya kwamba hapa, akiwa yupo mahali fulani, amesimama Bwana Yesu. Naye dada yetu ametoka mbali sana huku chini kuombewa. Ana matatizo ubavuni mwake, yuna wasiwasi. Lakini, Wewe, Bwana, uliyemfufua Yesu, na kufanya maandalizi. . .

268 Na huko nyuma, miaka mingi iliyopita, kama maskini mvulana mdogo, nikisimama kule chini ya mti, Wewe ulisema, “Kamwe usivute sigara, wala kunywa pombe, wala kuutia najisi mwili wako. Utakuwa na kazi ya kufanya utakapokuwa mtu mzima.” Hii hapa. Uliithibitisha kwa Malaika wa Nuru. Ulituma wanyama wakaombewe. Umepitia ulimwenguni kote pamoja na uamsho, kama ulivyoahidi hapa chini mtoni, ya kwamba ungelifanya.

269 Naye huyu hapa mwanamke huyu amesimama, leo, apate kukombolewa. Basi, Baba, kwa Damu ya thamani ya Yesu, kwa kuhubiriwa kwa Neno, ninaweka mikono juu ya dada na kumkomboa kulingana na Neno la Mungu na imani yake. Ninalaani kitu hiki kinachomsumbua, kivuli hiki cha kale cha giza kinachomtia wasiwasi. Ninakiondoa kwake, katika Jina la Bwana Yesu, nikichukua hatua.

270 Shetani, huwezi kumshikilia zaidi. Alikuwa kutoka mbali. Anarudi bila wewe. Umekwisha, kupitia Yesu Kristo Mwana wa Mungu.

271 “Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa huyo.” Ulisema hivyo, Mungu, naye atakuwa mzima. Tunamtoa adui sasa; omba Damu ya Bwana Yesu mwenye haki, kati yake na adui, katika Jina la Yesu.

272 Sasa, inaweza isiwe chochote kwa nje. Lakini wewe—wewe unajisikia kwamba umepona. Sivyo, dada? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Maumivu hayako ubavuni mwako. Yametoweka. Unajisikia mtulivu na mzima. Sasa papa hapa tu.

273 Huyu hapa mama. Unaweza kuinua kichwa chako. Kutoka Ohio, akiwa na tatizo hilo ubavuni mwake. Anasema, “Maumivu yote yametoweka.” Mishipa yake imetulia. Sawa tu na yule mwanamume. . . Hiyo ni kweli, dada? [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Sasa unaenda nyumbani kuwa mzima. Yesu, Mwana wa Mungu, ambaye yuko hapa asubuhi ya leo, amekuponya. Uwe mtumishi hodari Kwake. Mungu akubariki.

274 Sasa na tuseme, “Bwana asifiwe.” [Kusanyiko linasema, “Bwana asifiwe.”—Mh.] Vipi kama huyo alikuwa ni wewe ukiteseka hivyo? Vema.

275 Sasa na tuinamishe vichwa vyetu tena, katika ninii tu. . . kwa maombi mafupi. Vema.

276 Sasa tunaninii. . . ? . . . Sasa, naam, haja yako ni ipi? Loo. . . ? . . . Loo, naona ukishtuka. Loo, jamani! . . . ? . . .

Sasa, kila mtu awe na kicho sana, tafadhalini.

²⁷⁷ Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, maskini mama huyu anakuja, hajiwezi, kutoka kwa madaktari. Wamefanya yote wanayojua kufanya. Uso wake ukishtuka-shtuka, mishipa, kitu fulani kilienda kombo. Madaktari, wakijaribu kutafuta, lakini hawawezi kujua ni kwa nini mshipa huo hautafanya kazi vizuri. Na, katika hilo, yeye ni mgonjwa kila mahali. Kweli, Bwana, hiyo si ndiyo njia ya ulimwengu leo hii! Lakini, akijua jambo hilo, amesimama hapa, hajiwezi, Mbele Zako. Halafu, kama mtumishi Wako, ninamleta Kwako, kwa imani yote nijuayo. Na tukijua ya kwamba Shetani ndiye aliyevunja mshipa huo, kuna kitu fulani kisichoonekana ambacho madaktari hawawezi kuona, kinachosababisha mshipa huo kulishtusha jicho na uso wake. Lakini Wewe unaweza kukifanya kiondoke, Bwana, kwa maana Wewe ndiwe Yehova Mungu. Wewe Ndiwe uliyetoa dhabihu pale Kalvari, nasi tunaikubali sasa.

²⁷⁸ Nenda, ewe pepo, wewe unayeushtusha uso wake, wewe ambaye umeutesa mwili wake. Tunakuja katika Jina la Yesu, upya kutoka Kalvari, kutoka kwenye Neno, nasi tunakuhukumu. Tunatangaza kwamba huwezi kukaa tena. Huyu mwanamke amejaribu na madaktari, nao wamefanya yote wanayojua jinsi ya kufanya, lakini umejificha kutoka kwa madaktari. Ila huwezi kujificha kutoka kwa Mungu. Anajua wewe ni nani. Kwa hivyo, kama mtumishi Wake na mwakilishi Wake, nasema umwache dada yangu. Toka ndani yake. Neno la Mungu lilisema, “Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya,” kwa hiyo umeshindwa sasa katika upatanisho wa Kalvari. Ondoka kwa mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo. Ninamkomboa kutoka kwako, kwa agizo la Yesu Kristo, kwamba tunapaswa kuweka mikono juu ya wagonjwa na kuwatoa pepo wachafu. Nawe ni mchafu, na huna budi kumwacha. Naye aende nyumbani apate kupona, kupitia Jina la Yesu Kristo.

Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa kwa muda zaidi kidogo.

²⁷⁹ Sasa, Bibi Kinzer, naamini ndilo jina lako. Kusingekuwa na kitu hasa, imani yako tu, kukomesha hiyo mishtuko, kwa kuwa tumeomba, chini ubavuni. Lakini ninaamini, kwa moyo wangu wote, ya kwamba uko sawa, na ni mzima. Ilikuwa upande *huu* hapa ndani, moja kwa moja ndani ya uso wako. Sasa naomba uje hapa. Unatoka wapi sasa? [Dada huyo anasema, “Boston, Kentucky.”—Mh.] Boston, Kentucky.

Tafadhali inua kichwa chako.

²⁸⁰ Huyu mama, upande *huu* wa uso wake, alikuwa na kitu kutoka kooni kwenda chini hapa kikitetemeka, kikiruka juu chini, mshipa. Hiyo ni nini? Ni kama vile Biblia ilivyosema, “Pepo kiziwi akamtoka mtu.” Daktari asingeweza kuipata kwa sababu ilikuwa ni u—upasujaji wa mshipa. Mshipa huo ungali upo, lakini kuna kitu kwenye mshipa huo, kinachoufanya

kuruka na kuendelea. Madaktari hawangeweza kupata hicho, bila shaka, kwa sababu... [Dada huyo anasema, “Nimekuwa kwa kumi na watatu.”—Mh.] Amekuwa kwa madaktari kumi na watatu mbalimbali. Na sasa Yesu Kristo amelisimamisha, naye huyo hapo mbele yenu. Naye atapata afya. Atakuwa mzima sasa.

²⁸¹ Mungu akubariki, Dada Kinzer. [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Mungu akubariki.

²⁸² Hii imetokea kuwa ni siku yake ya kuzaliwa, naye alisema ni yenye furaha zaidi aliyowahi kuwa nayo. Mwangalie anaposhuka. Hiyo si ni ajabu sana? Hebu tuseme, “Mungu ashukuriwe.” “Mungu ashukuriwe!”

²⁸³ Sasa, tunampenda Bwana wetu Yesu mpendwa kwa moyo wetu wote. Hapa maskanini, tumejifunza kumpenda, na kumtumaini kwa kila kitu tunachohitaji.

²⁸⁴ Sasa, asante kwa kukiinamisha kichwa chako. Na sasa watamleta mgonjwa mwingine, huku ukiinamisha kichwa chako na kuwa katika maombi. Ni maombi yako pia.

²⁸⁵ Wewe ni... [Dada huyo anasema, “Bibi Brown kutoka Lima, Ohio.”—Mh.] Uh-huh. Na ni nini... [“...?...”] Hakika. Na shida yako ni nini? [“...?...”] Uh-huh. Je, wewe ni—wewe ni kiziwi au kitu fulani, katika ninii yako...?... [“...?...”] Uh-huh. [“...?...”] Naam, mama. [“...?...”] Kitu kama majipu au kitu fulani? Vema. Nawe unatoka Ohio?

²⁸⁶ Dada huyo anatoka mbali huko Ohio. Shida yake iko masikioni mwake. Yana ninii... Yanapasuka na kuvuja, na yanamletea shida nyingi sana. Nasi tunaamini kwamba Yesu anaweza kuishinda hii, au tayari ameishinda. Nasi tunakuja sasa kudai ushindi wake Kalvari.

²⁸⁷ Sasa, Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunamleta Kwako dada yetu mpendwa ambaye amekuja kutoka huko mbali Ohio, hapa, leo, kuponywa. Na kwa moyo wangu wote, na maombi marefu usiku kucha, nimekuomba, Bwana, kufanya mambo haya. Nami ninajua ya kwamba ni rahisi kukuomba Wewe, uliposema utafanya hivyo. Nami ni—ninashukuru sana kwamba umefanya hivyo.

²⁸⁸ Na sasa tunamleta Kwako, katika nuru ya msalaba wa Kalvari, ambapo Yesu, akiwa amesimama pale, aliyefanya u—upatanisho. Jinsi ulivyopembea kati ya mbingu na nchi, ukiwapatanisha walio wa Mbinguni na walio wa duniani, kwa kuimwaga Damu Yako Mwenyewe. Jinsi ulivyoinuliwa kutoka duniani! Ulikufia katikati ya anga. Na hapo Damu ikatiririka juu ya nchi, kutia doa msalaba wa kale wa Kalvari. Hapo ndipo ulipoharibu milki. Hapo ndipo ulipomnyang’anya Shetani kila kitu alichokuwa nacho. Ulichukua tena, na kuwapa watoto wa Mungu, mali yao halali. Hapo ndipo ulipotupa Uzima wa Milele. Hapo ndipo ulipotupatia ahadi ya ufufuo. Ee Baba wa Mbinguni, hiyo ililipa gharama!

²⁸⁹ Na, leo, umelipia uponyaji wake. Nami nasimama kama mtumishi Wako, pamoja na hawa mamia ya watumishi katika jengo hili. Nasi tunamlaani ibilisi huyu anayemtesa dada yetu. Na kusema, kupitia haki ya Kristo, kupitia amri Yake pale Kalvari, tunakutorosha kutoka kwa dada yetu. Na kumpeleka nyumbani kwake Ohio, haya yasichemke huko na kupasuka tena, hata atakuwa mzima kabisa. Kupitia Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, tunaomba. Amina.

²⁹⁰ Sasa, dada, kama... Kwa kweli, kuonyesha tu chochote, hungeweza, lakini unaamini, sivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo. Ninaiamini."—Mh.] Unaamini. Nataka utembe uje hapa.

²⁹¹ Sasa, kwako, unaweza kuinua kichwa chako. Dada yetu hapa hangeweza kuonyesha chochote, kwa sababu hayakuwa yanavuja kwa wakati huo, masikio yake. Lakini tunalo, asubuhi ya leo, hakikisho, moyoni mwangu na moyoni mwake, na, nina hakika, moyoni mwako, ya kwamba Mungu amemponya dada yetu. Je, unaamini hilo? [Dada huyo anasema, "Amina. Amina. Asante, Yesu."—Mh.] Na itakuwa ushuhuda.

Na Mungu akubariki, dada. Amina. Mungu ashukuriwe!

²⁹² Sasa na tuinamishe vichwa vyetu tena, tunapomwomba mtu mwingine.

²⁹³ Vema, dada, nakuona kwenye mkongojo wako, kwa hivyo najua kiasi hicho ndivyo ilivyo.

²⁹⁴ Sasa na tuombe. Inamisha kichwa chako, kwa muda kidogo, ninapozungumza na huyu dada.

²⁹⁵ Sasa, shida yako ni nini, dada? [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naam, mama. Na hii ni—ni huko kuyumbayumba, sivyo? ["...?..."]...?...Shinikizo kuu la damu. Naam, mama. Nawe ni Mkristo? ["Ndiyo, bwana."] Naam, mama. Na unaamini sasa ya kwamba umemjia Bwana Yesu, dada? ["Ndiyo."]

²⁹⁶ Sasa, dada yetu ana shida kwenye vifundo vya miguu. Anatembea kwa m—m—msaada wa mkongojo. Pia ana shinikizo la damu, na—na ana shida nyingi. Tunampeleka kwa Yesu, wakati huu, kwa ajili ya uponyaji wake. Iweni katika maombi sasa, maombi yenu yaweze kufika kwa ajili yake.

²⁹⁷ Sasa, Baba yetu mpendwa wa Mbinguni, dada yetu mpendwa amesimama hapa, angali ni msichana. Lakini, Shetani angempa kiharusi kama angeweza; angemlaza huko juu, juu ya kitanda cha mateso. Atamtoa kazini, akiweza, kwa maana hataki ushuhuda wake. "Kwa nini hili likamtokea Mkristo huyu? Kwa nini?" Tungeuliza, au wale ambao hawangeelewa. Lakini, Baba, tunajua ya kwamba ilikuwa kwa ajili ya utukufu Wako.

²⁹⁸ Ilisemekana wakati mmoja, "Ni nani aliyetenda dhambi; mvulana huyu, au mama yake, au baba yake?"

299 Ulisema, “Si yeyote, bali ili kazi za Mungu zidhihirishwe.”

300 Tunaamini jambo hilo kwa ajili ya dada yetu, asubuhi ya leo. Tunaamini hiyo ndiyo sababu vifundo vya miguu yake vikawa katika hali hiyo. Tunaamini hiyo ndiyo sababu shinikizo la damu lilimpata, ili umwonyeshe upendo Wako na fadhili kwake, ili uweze kumthibitishia ya kwamba Wewe ndiwe Yehova aponyaye magonjwa yetu.

301 Mungu, tunaomba kwamba shinikizo hili la damu lipungue hivi kwamba, hata daktari atasema, “Ni nini kilikupata?”

Kisha, kwa daktari, atasema, “Yesu aliniponya.”

302 Tunaomba, Mungu, ya kwamba utamfanya atembea kwa vifundo hivi vya miguu bila usaidizi huu. Kwamba ataweza kutembea na kuishi na—na kuwa jinsi vile anavyotaka kuwa. Na, Baba, Neno limetolewa, hata hivyo katika urahisi Wake na kukatakatwa, lakini hakika limeingia moyoni. . . mahali fulani mioyoni mwa Wakristo hawa. Na sasa amesimama hapa. Anangojea uponyaji wake. Wewe kamwe humpotezi mtu. Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utamponya dada yetu na kumpa afya.

303 Na sasa, kama mtumishi Wako, kama mtu anayekuamini Wewe, pamoja na hawa watumishi Wako wengine, ambao wameinama katika maombi. Tunamleta dada yetu hadi Kalvari; kule amening’inia Bwana Yesu. Loo, ni ajabu jinsi gani! Akisimama huko, ardhi chini Yake, mbingu juu Yake, akimpatanisha Mungu na mwanadamu pamoja. Nasi tunakuja katika Jina Lake.

304 Na kinachomzuia mwanamke huyu kuwa mtumishi aliyekombolewa kikamilifu ni ibilisi. Na hapo, Yesu, ulimvua nguo, na Wewe uko. . . ulichukua kila haki halali aliyokuwa nayo, ukamnyang’anya. Na leo hii yeye ni mdanganyifu tu, na hatutampokea. Hatutampokea, kwa sababu Yesu Kristo Mwana wa Mungu ametupatia sisi. . . alilithibitisha. Alitwambia tungeweza kufanya hivyo, nasi tunaamini. Na tunarudisha kile anachojaribu kumnyang’anya dada yetu. Tunampa afya yake. Tunaondoa udhaifu huu kutoka kwenye vifundo vyake. Tunarudisha shinikizo hili la damu katika hali yake ya kawaida, na kumkemea ibilisi aliyefanya hivyo, katika Jina la Yesu Kristo, kwa minajili ya mwanga wa dhabihu ya Kalvari.

305 Toka kwake, Shetani. Wewe ni mwovu, wala huwezi kumshikilia zaidi.

306 Na Wewe, Bwana, uliyetoa lile ono hivi majuzi usiku, na kusema, “Mambo haya yangekuwa.” Wewe ni wa Kweli, wala huwezi kushindwa. Nami ninaomba sasa kwa ajili ya ukombozi wa dada yetu, kupitia Jina la Yesu Kristo, ambaye atapokea sifa na utukufu wote.

Na vichwa vyenu vimeinamishwa, kila mtu.

307 Sasa, dada, kweli, kwa nje, mimi. . . jambo pekee ninaloweza kusema, ni kwamba uso wako, ambao ulikuwa mwekundu na usiovutia wakati ulipopanda hapa juu, umepungua. Sijui kama unahisi. [Dada huyo anasema, “Najisikia mtulivu zaidi.”—Mh.] Unajisikia mtulivu na umepoa. Na sasa hebu tuone mkongojo wako hapa, kidogo tu. Siamini itakubidi kuwa nao tena, tembea tu hapa bila huo. [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham.] Tembea tu, unaona, tembea tu hapa. Sasa hiyo ni sawa.

308 Sasa nataka ninyi nyote mtazame. Yule mama ambaye alikuwa amevimba uso wake wote, anajisikia mtulivu. Angalieni jinsi anavyoonekana sasa. Mliuona uso wake, jinsi alivyokuwa mwekundu. Na hapa yeye. . . Naye anajisikia mzima, ya kwamba Mungu amemponya na kumpa afya. Na, mkongojo wake, hatauhitaji huo tena, haijalishi yuko wapi.

309 Endelea kushuka, dada, chu—chukua tu kitu hicho na ukibebe, nimepata. . . utundike nyumbani mwako kwa ajili ya ukumbusho, unaona, haitakubidi kuutumia.

310 Hebu tuseme, “Bwana asifiwe.” [Kusanyiko linasema, “Bwana asifiwe.”—Mh.]

Vema, na tuinamishe vichwa vyetu tena sasa kwa maombi.

Sawa, naomba umlete huyo dada.

311 Na shida yako ni nini, dada? [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Loo. [“...?...”] Loo. Unatoka wapi? [“Madisonville, Kentucky.”] Madisonville, Kentucky. Bibi Jackson.

312 Dada huyu ana yabisi kavu, na shida zingine za ndani ambazo ni mbaya sana. Nami sijui itakuwaje endapo Mungu hatamponya. Labda itabidi afanyiwe upasuaji, na hiyo ni hatari sana wakati huu, hivyo tunaomba kwamba Mungu atamrehemu na kumponya.

313 Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunamleta Kwako, leo, dada yetu mpendwa, ametoka mbali huko Madisonville, Kentucky, akaja hapa kuombewa. Nawe ndiwe Mponyaji, wa Kiungu. Nami namleta katika uweza Wako wote, na katika Uwepo Wako mkuu, ninii yake. . . Nguvu Zako na Uwepo wako, kukemea ugonjwa huu wa yabisi kavu ambao ungeweka kalisi kwenye mifupa hii ya vidole vyake, ambao ungeweka kalisi kwenye vifundo hivi na magoti.

314 Huyu hapo, amelazwa kitandani, mtu akimlisha kupitia tyubu. Loo, ewe pepo mchafu, ungesababisha kuondolewa kwa uhai wake, kutokana na udhaifu huu mwingine. Lakini tunamleta, leo, kwa Yesu Kristo.

315 Na, Ee Mungu, kuongeza imani yangu mwenyewe kwa ajili yake sasa, nikijua ya kwamba maombi ya imani yameombwa! Ninamhukumu ibilisi, ninamtoa kwake, kwa njia ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu; kumkomboa kutokana na yabisi kavu na

magonjwa haya mengine yote, ili aweze kwenda nyumbani na kuwa mzima, na kutoa ushuhuda kote katika nchi hiyo, wa utukufu wa Mungu.

³¹⁶ Shetani, umepoteza ushindi, naye Yesu Kristo ameshinda. Na hebu awe mzima, kupitia Yesu Kristo. Amina.

³¹⁷ Dada, mpenzi, huenda kusiwe na kitu ambacho watu wangeweza kuona, lakini ninaamini ya kwamba umeponywa. Inua miguu yako, uone tu kama unajisikia vizuri zaidi, kutokana na yabisi kavu yako. Unajisikia vizuri sasa? Sasa nyote mnaweza kuona jinsi anavyosogeza miguu yake, karibu mnaweza. Tembea ushuke chini moja kwa moja sasa, kama tu msichana mdogo, kwamba tu hata hutaninii. . .

³¹⁸ Tunamsifu tu Bwana Yesu kwa wema na rehema Zake zote!

³¹⁹ Sasa iweni na kicho, kila mmoja, tunapoomba. Na sasa kidogo tu, nasi. . .punde tunapomwombea mtoto huyu, ndipo tutapumzika kidogo, halafu mnaweza kwenda. Itatuchukua yapata dakika tatu sasa, kisha tutapumzika kidogo, halafu tutaanza na watu wengine zaidi. Vema. Kila mtu awe tu na kicho sana sasa. Vema.

³²⁰ Je, ni mtoto mchanga anayetaka kuombewa? Nawe unataka kuombewa, pia? Ndugu Wilson, nina furaha kupata kukupa mkono. Na mtoto wako ni. . .[Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Loo, sawa. Loo, naam, sawa. Ni yule ambaye ana kitu kama kifafa. Huanguka. Naona aliuponda uso wake mdogo, kule juu. Vema, basi, dada, utaamini, na wewe, Ndugu Wilson, leo kwamba Yesu atakiondoa hiki kutoka kwa mtoto wenu, na—na kumpa afya?

³²¹ Sasa, mtoto mchanga anayesimama hapa, ana shida fulani. Alikuwa na kifafa, hata huanguka. Na maskini uso wake, macho yake madogo, yamechubuliwa na ni meusi, na kadhalika. Naye baba anataka uponyaji, pia. Sasa, tunaomba ya kwamba Mungu ataiondoa laana hii kutoka kwa mtoto huyo mchanga.

³²² Sasa, wasikilizaji, mnaamini kwamba Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, katika rehema Zake, atamjaliza mtoto huyu mdogo apate afya, asiwe na vipindi hivi vya kifafa hiki, kwamba vitamwacha? Je, unaamini, tukimwomba Baba yetu wa Mbinguni, atafanya hivyo? Vema.

Na tuombe.

³²³ Na, Ndugu Wilson, shida yako ilikuwa nini? Nilisahau. [Ndugu Wilson anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Uhuh. Sawa. Pengine ni tatizo lile lile alilo nalo huyo mtoto mchanga, pia.

Vema, sasa hebu sote na tuwe na kicho sana.

³²⁴ Sasa, Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunamleta Kwako, kwanza, kama wa kwanza kuja ulimwenguni, baba wa mtoto mchanga. Na mambo mabaya yamempata. Ibilisi

amemshinda katika nyakati nyingi kuu. Lakini, leo, tunamleta Uweponi mwa Yesu Kristo, kwa njia ya maombi. Tunamleta Kalvari, ambapo, pale ambapo Yesu alikufa ili apate kuwa na hisi tano kamili. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utamrehemu. Kwamba, tunaamini ya kwamba mambo haya tunayofanya ni kulingana na Neno Lako. Ulisema, “Kwa Jina Langu watamtoa pepo mchafu.” Tunaamini hilo. Ingawaje, nyakati, watu. . .

³²⁵ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . waliniambia jambo fulani la kufanya, na wengine jambo la kusema. Nami sikuweza kamwe kukumbuka kile alichosema, nilipoamka. Unakumbuka hilo. Hivi majuzi usiku, katika ono, alipozungumza nami, “Nayo mambo haya hayakupaswa kufanywa hadharani. Yanapaswa kufanywa faraghani.” Naye Ndugu Cox, ambaye amesimama karibu, tulipendekeza, labda ingekuwa bora kuwaacha watu waje *huku*, kuniruhusu kuwa na mtu mmoja kwa wakati mmoja, katika—katika chumba cha maombi hapa, ili hili lifanyiike.

³²⁶ Jumapili iliyopita, nilipokuwa hapa, nilikuwa nikifanya jambo hili kwanza maskanini. Niliwafanya watu wote wainamishe vichwa vyao, ili niweze kushuka chini kwa mwanamke huyu ambaye alikuwa kiwete, aliyelazwa kwenye machela hii. Naye akakombolewa kikamilifu.

³²⁷ Ndipo asubuhi ya leo, nilisema, “Mungu, kama utanisaidia tu kwa muda kidogo, mpaka umati utakapohangaika. Vema, nisaide, mpaka, labda kama ninaweza kuwaweka watu wameinamisha vichwa vyao, ili wasione likitendeka.” Mnaona? Kila mtu. . .

³²⁸ Basi nilipoweka . . . nilipoanza kuweka mikono yangu juu ya watu, ndipo kila mtu akaanza kusema “Loo, ninaihisi mkononi mwangu.” Mnaona, namna hiyo. Ndipo wakati ilipokuja, basi kila mtu akaanza . . . Mnaona jinsi ilivyokuwa? Ambayo ilikuwa ni uigaji wa kimwili kabisa. Hiyo ni kweli kabisa. Roho Mtakatifu yeye yule aliyeniambia nifanye hivyo, alisema ndivyo ilivyokuwa. Kwa hiyo nilijua haikuwa sahihi.

³²⁹ Kwa hiyo hapo ndipo aliponiambia hivi majuzi usiku, kasema, “Ulisababisha uigaji mwingi wa kimwili kuinuka, na kufanya jambo hilo.” Kasema, “Sasa usiache mtu yeyote aone hili.”

³³⁰ Na hivyo ndivyo nimekuwa nikifanya asubuhi ya leo, kusudi ninyi nyote mjue. Mngeona sasa kwamba nimewaambia ukweli.

³³¹ Angalieni tu sasa kile Bwana atakachofanya katika miamsho hii inayokuja. Yatakuwa kwa wingi, makubwa kuliko chochote ambacho kimewahi kufanywa bado. Angalieni tu sasa. Kumbukeni, mimi si nabii wa uongo. Nasema ukweli. Mungu asingesema uongo. Basi angalieni kama hayatakuwa makubwa kuliko yalivyowahi kuwa wakati wowote.

332 Sasa, ninyi watu wapendwa, kuna wengi wenu waliojipanga hapa ili kuombewa. Kunachelewa. Nitaninii... Na—nami na—najua mnataka kuombewa. Nami nataka kuombea mambo haya. Huyu mama ana msichana mdogo aliyesimama hapa; na mama aliyemshika mtoto mchanga; na—na wote; nasi tunataka waombewe. Tunataka wakombolewe, sivyo? Tunataka waponywe, kila mmoja; hawa wavulana wadogo walipiga magoti hapa; na wote huko nyuma, watu; na watu hapa wakiwa na kansa, na hali mbaya, nao watakufa.

333 Sasa, hivi hatuamini kwamba Yesu yuko hapa sasa? Je, hatuamini kwamba Yeye yuko hapa? Nasi tunaamini, kwa moyo wetu wote, ya kwamba atamponya kila mmoja wetu. Je, hamwamini hivyo? Anatupenda sisi sote. Mungu hana upendeleo.

334 Yeye atamponya huyu msichana mdogo, sivyo, dada pale uliye na huyo msichana? Yeye... [Dada huyo anasema, "Tayari ameanza."—Mh.] "Tayari ameanza!" Nakutakia heri! Unatoka wapi dada? ["Crestwood."] Crestwood, Kentucky. ["Mwanamume *huyu* hapa alimwomba, usiku mmoja, naye amekuwa akipata nafuu tangu wakati huo."]

335 Loo, hebu tuseme, "Bwana asifiwe." [Kusanyiko linasema, "Bwana asifiwe."—Mh.] Ndugu Neville alikuja, akaomba, msichana huyu mdogo.

336 Vema, rafiki msiri wangu hapa, Ndugu Wood, anatoka Crestwood. Na ninii yake... Unawajua, Ndugu Wood, unawajua? Huh? [Ndugu Wood anasema, "Naam."—Mh.] Uh-huh! Yeye ni kontrakta huko.

[Dada huyo anasema, "Nimemwona huko."—Mh.] Naam.

337 Naye mtoto huyu mchanga hapa, ametoka wapi, dada? [Dada huyo anasema, "Gary, Indiana."—Mh.] Gary, Indiana. Na unaamini ataninii, atarudi—atarudi Gary na apone, sivyo? ["Loo, ndiyo."] Hakika, unaamini. Vema.

338 Nao hawa wavulana wadogo wametoka wapi? [Ndugu mmoja anasema, "Austin, Indiana."—Mh.] Austin, Indiana. Mnaamini mtarudi na kuwa wazima, leo, pia, sivyo? Hakika, tunaamini.

339 Je, huyo mtoto mchanga ni wa kuombewa, dada? Unatoka wapi? [Dada huyo anasema, "Indiana."—Mh.] Indiana. Wapi? ["New Albany."] New Albany. Unaamini huyo mtoto mchanga atapona? Hakika.

340 Basi mnaamini watu hawa wengine wote watapona hapa, kila mtu? Sasa hebu tujifunge pamoja, na kusema, "Yesu Kristo, Wewe u hai na unatawala!"

341 Loo, wazia ukuu wa Bwana Yesu; Yule aliyeweza kufanya macho ya mtoto huyo kipofu kabisa yafunguke; Yule aliyeweza kumfanya mtu huyo mwenye kigugumizi ambaye... [Ndugu

Branham anaiga kugogota maneno—Mh.] . . . na kusimama hapa na kuzungumza kwa ujasiri na kawaida, ni Nani angeweza kufanya mambo haya mengine yatendeke? Mungu ni Mungu, sivyo?

³⁴² Hayo ni mambo madogo, ukilinganisha na yale atakayofanya. Yeye atafanya tu mambo makuu, makuu, na ataendelea tu kuyafanya mpaka atakapokuja. Hiyo ni kweli.

³⁴³ Sasa nitawaambia msimamo wa kuingia. Ingia kwenye msimamo huu, “Yesu, uko hapa. Sasa ninakubali uponyaji. Ninauamini kwa moyo wangu wote. Na sasa imekwisha.”

³⁴⁴ Na moyoni mwako, kama vile tu ulivyomjia upate kuokolewa, useme, “Bwana Yesu, natoa yangu yote. Hakuna kitu cha zaidi ninachoweza kufanya. Huu hapa moyo wangu. Haya hapa maisha yangu. Ninajitoa Kwako.” Hayo ndiyo yote ambayo yanaweza kufanywa. Kisha useme, “Ninaamini, Bwana Yesu.”

³⁴⁵ Na mara moja, kitu Fulani hapa chini kinasema, “Naam, unaamini. Naam, unaamini.”

³⁴⁶ Mtoto wako mchanga amekuwa mgonjwa kwa muda gani, ndugu? [Mama anasema, “Tangu alipozaliwa.”—Mh.] Tangu alipozaliwa. Shida yake ni nini? [Baba anasema, “Amedumaa.”] Ati kudumaa? Angalia, unajua ibilisi alifanya hilo. Hiyo ni kweli. Ibilisi alifanya hilo. Mungu anaweza kumfanya mtoto huyo mchanga mzima tena. Wazia tu, nimeona wagonjwa kadhaa wa huo, ambao ni wazima kabisa na wamepata afya sasa. Nami nataka . . . najua. Nina mtoto mdogo, pia, nami ninajua jinsi unavyojisikia. Basi uwe tu na moyo wa ushujaa.

³⁴⁷ Nyote wawili ni Wakristo? Hakuna yeyote wenu aliye Wakristo? Je, mtamtotea Yesu maisha yenu, asubuhi ya leo, mkisimama hapo, na kuahidi kumwishia Yeye, ikiwa Mungu atamruhusu mtoto wenu mdogo apone na kuwa mzima? Utafanya hivyo, sivyo, ndugu? Utafanya hivyo. Utafanya hivyo, sivyo, dada? Mungu awabariki. Sasa mnakuwa Wakristo mnapomkubali Bwana Yesu kama Mwokozi wenu. Sasa tunamkubali kama mponyaji wa huyu mtoto mchanga.

³⁴⁸ Sasa, Baba wa Mbinguni, ninapoweka mikono juu ya mtoto huyu mdogo aliyebarikiwa. Ambapo watoto wawili waliozaliwa hivi punde wamekuja, baba na mama. Na ilibidi kumchukua mtoto huyu, kuwaleta kwenye Uzima wa Milele. Labda, isingalikuwa huyu mtoto mchanga kuwa hivi, wangepotea milele. Lakini huyu mtoto mchanga amekuwa mwokozi wa muda, au mdogo kwao, ili kuwaleta kwa Bwana Yesu, kwa ajili ya wokovu wao. Tunakushukuru Wewe, Baba. Na sasa wabariki.

³⁴⁹ Wao ni watoto Wako. Wanakukubali. Ulisema katika Neno Lako, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele na hataingia hukumuni.” Nikiwaangalia hawa mume na mke wachanga hapa, na kuona

Nuru hiyo ikining'inia juu yao, nilipoanza kwenda mwisho wa mstari. Na kuona Nuru hiyo ikining'inia juu ya hawa mume na mke wachanga, niliona ni vyema kuzungumza nao, Baba. Sio kwamba kusanyiko lisikie, bali Wewe peke yako. Na sasa ilikuwa nini? Ilikuwa ni Wewe ukivuta moyoni mwao, katika wakati huo muhimu sana. Ee Mungu, tunashukuru sana wao ni Wakristo.

³⁵⁰ Tunambariki mtoto wao mchanga, katika Jina la Yesu Kristo. Tumekuja kwa sababu Mungu alisema, ama Yesu alisema, katika Neno Lake, “Mwombeni Baba lolote mtakalo, katika Jina Langu, nitalifanya.” Na kwa hiyo tunamwomba Baba, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanawe, ya kwamba atambariki mtoto huyu mchanga. Na jalia kuwe na mabadiliko makubwa katika mtoto huyu mchanga, katika saa ishirini na nne zijazo, mpaka baba na mama watashangilia na kujua yaliyotokea, kujua kwamba Bwana wao Yesu waliyempata upya anamponya mtoto wao mchanga. Tujalie, Bwana. Ninazikemea kazi za ibilisi, dhambi zinaungamwa. Baba na mama ni Wakristo.

³⁵¹ Sasa, Shetani, huna haki tena. Yote yamekwisha. Kwa hiyo, tunakushinda kwa Damu ya Yesu Kristo, aliyetuamuru kufanya hivyo, nasi tunakutupa mbali na mtoto huyu.

³⁵² Na sasa jalia aanze kukua na kusitawi, na—na kuwa mzima na mwenye afya, na kufanyika mtoto mzuri ambaye atawafanya baba na mama wamjivunie. Katika Jina la Yesu tunafanya baraka hii. Amina.

³⁵³ Ninyi ni Wakristo sasa, nyote wawili, katika Kristo. Angalieni tofauti ya mtoto wenu mchanga. Nanyi mnaishi wapi sasa? [Baba na mama wanasema, “Gary, Indiana.”—Mh.] Gary, Indiana. Niandikieni, au mnipigie simu, katika—katika siku nne au tano zijazo. Na mwangalie ni tofauti gani mnayoona kwa huyu mtoto, mtakaporudi nyumbani!

Na tumshukuru Mungu kwa kazi hii nzuri sana.

³⁵⁴ Nilianza kushuka hapa hadi mwisho wa mstari, na kuanza kuomba. Niliendelea kuona upako upo hapa kwa wingi sasa hivi. Mnaona, unawaangalia watu, na kadhalika. Lakini kwa namna fulani ninafanya jambo hilo kama jambo la pili, kuliweka upande mmoja, mpaka itakaponibidi; kama juu ya yule mwanamke muda mfupi uliopita. Lakini niliiona ikining'inia juu ya hao mume na mke, nami nikaendelea kushangaa ilikuwa wapi. Ndipo nikawazia, “Hapo ndipo ilipokuwa, moja kwa moja kwa watu hao hapo.”

³⁵⁵ Kwa hiyo, sasa, tutamwombea kila mtu. Kila mmoja wenu ataombewa, mradi tu... Mungu akinijalia kuishi. Nasi tutaanza na kuomba, ili tuweze kwa namna fulani kuondoka. Tukifikia hapa mwishoni mwa mstari.

³⁵⁶ Ndugu Fleeman, una...imetayarishwa hapo ili tuweze kupita?

³⁵⁷ Sasa nitashuka kule na kumwombea kila mtu. Nami nataka mpite, mkishangilia, na kumshukuru Mungu kwa uponyaji wenu. Amina.

³⁵⁸ Kwa watu, walio karibu, tazameni kipindi cha Ndugu Neville, Jumamosi ijayo, yapata—yapata...kwa ibada ya Jumapili hii ijayo, kama nikirudi kwa wakati kwa ajili ya Jumapili ijayo. Vema. 

56-0108 Mungu Anayo Njia Iliyoandaliwa
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org